JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2021

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P 2624,
Dar es Salaam.

**APRILI 2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2021

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P 2624,
Dar es Salaam.

**APRILI 2022**

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................................ vi

ORODHA YA CHATI ................................................................................ vii

ORODHA YA VIELELEZO.......................................................................viii

DIBAJI ....................................................................................................... x

SURA YA KWANZA...................................................................................1

SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU ....................1

1.1 Utangulizi ....................................................................................1
1.2 Sampuli ya Upimaji.........................................................................1
1.3 Mipaka ya Upimaji ........................................................................2
1.4 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji ..................................................2
1.5 Uchambuzi wa Takwimu na Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Stadi za KKK 2021 ..........................................................................2

SURA YA PILI ..........................................................................................4

UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA ................................................................4

2.1 Utangulizi ....................................................................................4
2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi za Kusoma .......................4
2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi za Kusoma ....................................5
2.4 Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi za Kusoma ................................6
2.4.1 Swali la 1 : Umahiri wa Kusoma Maneno ..........................................6
2.4.2 Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma kila Neno ............................10
2.4.3 Swali la 2 : Umahiri wa Ufahamu wa Kusoma na Kusikiliza .............13
2.4.4 Utendaji wa Wanafunzi katika kila Kipengele cha Ufahamu.............18
2.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo na Jinsi ..........................................................................20
2.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa kwa Mwaka 2019 na 2021 ..........................................................................................20
2.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo ..........................................................................................22
2.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi .............23
2.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi za Kusoma...........................24

SURA YA TATU.......................................................................................25

UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA ...........................................................25

3.1 Utangulizi ...................................................................................25

3.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi za Kuandika....................25
3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi za Kuandika ................................25
3.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Stadi za Kuandika .......26
3.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kutambua na Kuandika Jina la Picha Husika ..........................................................................................................26
3.4.2 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi katika kila Neno ..................35
3.4.3 Swali la 2 : Kuandika Maneno kwa Herufi Kubwa ............................40
3.4.4 Swali la 3: Kunakili Kifungu cha Maneno na kuweka Alama za Uandishi ............................................................................................47
3.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi za Kuandika kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo (Mijini/Vijijini) na Jinsi (Wavulana/Wasichana) ...................................................................52
3.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa kwa mwaka 2019 na 2021 .................................................................................................52
3.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi za Kuandika kwa Kuzingatia Mahali Shule Zilipo ........................................................54
3.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi .............55
3.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi za Kuandika.........................56

SURA YA NNE ......................................................................................58

UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU.....................................................58

4.1 Utangulizi ..........................................................................................58
4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji.......................................................58
4.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi za Kuhesabu ................................59
4.4 Utendaji wa Jumla katika Stadi za Kuhesabu..................................59
4.5 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi kwa kila Umahiri ................60
4.5.1 Umahiri wa Wanafunzi wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mfululizo wa Namba.........................................................................60
4.5.2 Umahiri wa Wanafunzi katika Kujumlisha.........................................64
4.5.3 Umahiri wa Wanafunzi katika Kutoa.................................................65
4.5.4 Umahiri wa Wanafunzi katika Kufumbua Mafumbo ..........................67
4.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi .............73
4.6.1 Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia Jinsi katika Upimaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo .....................................73
4.6.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Jinsi katika Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa ........................................................................74
4.7 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo.................................................................................................75
4.7.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo

kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini ........................................75
4.7.2 Ulinganifu wa Utendaji katika Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa Namba kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini .............................76
4.7.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo kati ya Mwaka 2019 na 2021 .........76
4.7.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa katika Kujumlisha na Kutoa Namba kati ya Mwaka 2019 na 2021 ....................................78
4.7.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Ujumla Kimikoa Mwaka 2019 na 2021 ...........................................................................80
4.8 Muhtasari wa Utendaji katika Stadi za Kuhesabu.............................82

SURA YA TANO ..........................................................................................84

HALI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) SHULENI ..................................................................84

5.1 Utangulizi .............................................................................................84

5.2 Mbinu iliyotumika kupata Taarifa ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK ...............................................................................................84

5.3 Taarifa Kuhusu Walimu na Wanafunzi ............................................84

5.4 Hali ya Upatikanaji wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia.84

5.5 Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji KKK.....................................86

5.6 Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK........87

SURA YA SITA.............................................................................................89

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..................................................................89

6.1 Utangulizi ..............................................................................................89
6.2 Hitimisho ...............................................................................................89
6.3 Mapendekezo.........................................................................................90

Kiambatisho Na. 1: Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma na Kuhesabu .92

Kiambatisho Na. 2: Skeli ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma na Kuhesabu ......96

Kiambatisho Na. 3: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika.........................105

Kiambatisho Na. 4: Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu ..................109

Kiambatisho Na. 5: Dodoso la Mkuu wa Shule...........................................112

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Utendaji wa Wanafunzi Waliofanya Upimaji Mwaka 2021..3
Jedwali Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ................6
Jedwali Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali ya Ufahamu ..........................................................................14
Jedwali Na. 4: Utendaji wa Jumla wa wanafunzi katika Stadi ya Kuandika ..........................................................................26
Jedwali Na. 5: Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu...................59
Jedwali Na. 6: Maswali ya Kujumlisha....................................................64
Jedwali Na. 7: Umahiri wa Kufumbua Mafumbo......................................67
Jedwali Na. 8: Hali ya Upatikanaji wa Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia ..........................................................................85
Jedwali Na. 9: Hali ya Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji..................86
Jedwali Na. 10: Changamoto Katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK..........................................................................87

## ORODHA YA CHATI


Chati Na. 1: Utendaji wa wanafunzi katika kusoma kila neno. .................... 11
Chati Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kila Kipengele cha Swali la 2. . 19
Chati Na. 3: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimkoa ........................ 21
Chati Na. 4: Utendaji wa Wanafunzi Wanaosoma Shule za Mjini na Wanaosoma Shule za Vijijini. ................................................ 22
Chati Na. 5: Ulinganifu wa Utendaji Kati ya Wavulana na Wasichana. ....... 23
Chati Na. 6: Utendaji wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha. ........ 27
Chati Na. 7: Utendaji wa wanafunzi katika kuandika maneno kwa herufi kubwa. ........................................................................ 40
Chati Na. 8: Utendaji wa wanafunzi katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. .................................................. 48
Chati Na. 9: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa kwa mwaka 2019 na 2021. ....................................................................... 53
Chati Na. 10: Utendaji wa wanafunzi kwa shule za mjini na vijijini. ............... 55
Chati Na. 11: Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia Jinsi. .......................... 56
Chati Na. 12: Asilimia ya wanafunzi walioweza kutambua namba inayokosekana kwenye mfululizo wa namba. ......................... 61
Chati Na. 13: Asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali ya kujumlisha namba. ................................................................ 65
Chati Na. 14: Asilimia ya wanafunzi walifanya kwa usahihi tendo la kutoa namba. ................................................................................. 66
Chati Na. 15: Asilimia ya wanafunzi waliofumbua mafumbo yaliyotolewa kwa usahihi. ........................................................................... 68
Chati Na. 16: Matokeo ya jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa jinsi. ............. 73
Chati Na. 17: Matokeo ya jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa Jinsi. ............ 74
Chati Na. 18: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini. ........................................................................... 75
Chati Na. 19: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini katika kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa. .............. 76
Chati Na. 20: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika kutambua namba na Kufumbua mafumbo kimikoa mwaka 2019 na 2021 .......... 77
Chati Na. 21: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika kujumlisha na kutoa kimikoa. ........................................................................ 79
Chati Na. 22: Ulinganifu wa jumla wa utendaji wa wanafunzi kimikoa. ......... 81

## ORODHA YA VIELELEZO


Kielelezo Na. 1: Sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika swali la 1. ........................7
Kielelezo Na. 2: Sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika swali la 1. ........................7
Kielelezo Na. 3: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 1. ........................8
Kielelezo Na. 4: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 1. ........................8
Kielelezo Na. 5: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji mzuri katika swali la 1. ........................9
Kielelezo Na. 6: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani katika swali la 1. ........................9
Kielelezo Na. 7: Sampuli ya majibu ya wanafunzi mwenye utendaji hafifukatika swali la 2. ........................15
Kielelezo Na. 8: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji hafifu katika swali la 2. ........................15
Kielelezo Na. 9: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji mzuri katika swali la 2. ........................16
Kielelezo Na. 10: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani katika swali la 2. ........................17
Kielelezo Na. 11: Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji mzuri sana katika swali la 2. ........................18
Kielelezo Na. 12: Sampuli ya jibu lisilo sahihi........................29
Kielelezo Na. 13: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani. ........................31
Kielelezo Na. 14: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri. ....33
Kielelezo Na. 15: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana. ........................35
Kielelezo Na. 16 (a): Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika herufi ya kwanza kwa kila neno alilopewa. ........................42
Kielelezo Na. 16 (b): Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyetunga sentensi kwenye baadhi ya majibu yake badala ya kuandika maneno aliyopewa kwa herufi kubwa. ……………………………………….. 43
Kielelezo Na. 16 (c): Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika baadhi ya majina ya picha katika swali la kwanza badala ya kuandika majina husika kwa herufi kubwa …………. ..44
Kielelezo Na. 17: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji

wa wastani…………………………………………………45
Kielelezo Na. 18: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri…………………………………………………46
Kielelezo Na. 19: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana……………………...................................47
Kielelezo Na. 20 (a): Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi..........49
Kielelezo Na. 20 (b): Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi..........49

Kielelezo Na. 21: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani. ..................................................................50
Kielelezo Na. 22: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri. .........................................................................51
Kielelezo Na. 23: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana...................................................................52
Kielelezo Na. 24: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana...................................................................62
Kielelezo Na. 25: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani. ..................................................................62
Kielelezo Na. 26: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji hafifu. ........................................................................63
Kielelezo Na. 27: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa. ....................................69
Kielelezo Na. 28: Sampuli ya kazi ya mwanafunzi aliyejibu maswali ya mafumbo kwa usahihi. ................................................70
Kielelezo Na. 29: Sampuli ya majibu mwanafunzi aliyeshindwa kufumbua mafumbo yote. ............................................................72

## DIBAJI

Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Pili mwaka 2021 uliendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa lengo la kubaini umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi hizo. Upimaji huo ulifanyika tarehe 24 Januari, 2022 na 25 Januari, 2022 kwa wanafunzi waliokuwa Darasa la Pili mwaka 2021. Upimaji ulifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo jumla ya shule 524 za Msingi za Serikali kutoka katika Halmashauri zote 186 ziliteuliwa kushiriki. Aidha, shule 2 hadi 5 ziliteuliwa kutoka kila Halmashauri kwa kuzingatia idadi ya shule katika Halmashauri na maeneo ya vijijini na mijini.

Zana za upimaji kwa Stadi zote tatu ziliandaliwa na Baraza la Mitihani. Stadi za Kuandika na Kuhesabu zilipimwa kwa kutumia karatasi za upimaji kwa shule zote 524. Aidha, jumla ya shule 489 zilitumia Skeli ya Upimaji kurekodi alama za Stadi za Kusoma na Kuhesabu ambayo ilifanyika kwa njia ya mdomo wakati shule 35 zilitumia Vishikwambi katika kurekodi alama za upimaji wa stadi hizo. Vilevile, Walimu Wakuu, Wasimamizi Wakuu na Wasimamizi wa Mikondo walioteuliwa kusimamia upimaji walijaza dodoso kuhusu hali ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK.

Jumla ya wanafunzi waliosajiliwa kufanya upimaji wa Stadi za KKK ni 28,364. Kati yao, wanafunzi 27,770 sawa na asilimia 97.90 walifanyiwa upimaji ambapo wanafunzi 594 sawa na asilimia 2.10 hawakufanyiwa upimaji huo kutokana na sababu mbalimbali.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanyika ili kubaini viwango vya utendaji wao katika kila stadi. Uchambuzi huo unaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi walioshiriki upimaji ulikuwa wa wastani katika stadi zote tatu kwa asilimia 63.73. Stadi za Kusoma zilikuwa na utendaji wa juu zaidi kwani asilimia 68.10 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na Stadi za Kuandika (62.21%) na Stadi za Kuhesabu (60.90%).

Taarifa hii imegawanyika katika sura sita. Sura ya Kwanza ni Utangulizi, Sura ya Pili hadi ya Nne zinaelezea Uendeshaji na Matokeo ya Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu mtawalia. Sura ya Tano inahusu Matokeo ya Uchambuzi wa Madodoso na Sura ya Sita inatoa Maoni, Mapendekezo na Hitimisho.

Baraza la Mitihani lina matumaini kuwa taarifa hii itatoa mrejesho muafaka kwa wadau wa Elimu wakiwemo walimu wanaofundisha Stadi za KKK kuhusu changamoto zinazowakabili wanafunzi katika kujifunza Stadi hizo nchini. Hivyo, inatarajiwa kuwa hatua sahihi zitachukuliwa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kuimarisha umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi hizo.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# SURA YA KWANZA

# SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU

## 1.1 Utangulizi

Baraza la Mitihani la Tanzania liliendesha upimaji kwa wanafunzi wa Darasa la Pili mwaka 2021 katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) tarehe 24 Januari, 2022 na 25 Januari, 2022. Upimaji huo ulilenga kubaini uwezo wa wanafunzi katika stadi hizo.

Umahiri wa wanafunzi ulipimwa katika dhana mbalimbali kwa kila stadi. Kwa mfano, katika Stadi za Kusoma, wanafunzi walipimwa umahiri wa kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha na haraka pamoja na kujenga ufahamu wakati wa kusoma na kisha kujibu maswali. Vilevile, katika Stadi za Kuandika, umahiri wa wanafunzi ulipimwa kwa kuzingatia uundaji wa maneno kwa kutumia picha, kubainisha maneno yaliyoandikwa kwa kutumia herufi kubwa na ndogo. Vilevile, walipimwa katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Aidha, katika Stadi za Kuhesabu, umahiri wa wanafunzi ulipimwa kwa kuzingatia uwezo wa kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba, kujumlisha au kutoa namba zisizozidi 999 pamoja na kufumbua mafumbo.

## 1.2 Sampuli ya Upimaji

Upimaji wa Darasa la Pili wa Stadi za KKK ulifanyika katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza na Njombe. Mikoa mingine ni Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga. Jumla ya Halmashauri 186 za mikoa hiyo nchini zilishiriki katika upimaji. Aidha, shule zote zilizoshiriki katika upimaji ziliteuliwa kwa njia ya sampuli nasibu kwa kuzingatia uwakilishi wa maeneo ya mijini na vijijini. Kati ya Shule 2 hadi 5 ziliteuliwa kwa kila Halmashauri na kufanya idadi ya shule zilizopimwa kuwa 524. Shule hizo ziliteuliwa miongoni mwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia. Jumla ya wanafunzi 27,214 walipimwa katika Stadi za Kuandika na Kuhesabu kwa kuandika wakati wanafunzi 27,770 walipimwa katika Stadi za Kusoma na Kuhesabu kwa kutamka. Mahudhurio ya wanafunzi katika upimaji huo yalitofautiana kati ya stadi moja na nyingine kutokana na utoro au ugonjwa.

### 1.3 Mipaka ya Upimaji

Katika upimaji huu, kulikuwa na mipaka ya upimaji iliyozingatiwa wakati wa kuteua sampuli iliyotumika. Mipaka hiyo ilikuwa ni pamoja na kuteua shule 524 kati ya 16,406 za Tanzania Bara kwa njia ya sampuli nasibu ili kufanya upimaji. Vilevile, shule zilizoteuliwa hazikuhusisha shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia na kujifunzia. Aidha, data zilizotumika kukokotoa utendaji wa wanafunzi katika kila stadi hazikuwekwa kwenye mizania (weighting), hivyo uchambuzi ulifanyika kwa kutumia data halisi.

### 1.4 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji

Zana za upimaji zilizotumika ni karatasi za maswali ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na madodoso (Tazama Viambatisho 1 hadi 5). Maswali yaliyoandaliwa kwa kila stadi yalipima umahiri wa wanafunzi kwa kuzingatia viwango vya utendaji. Aidha, kulikuwa na madodoso yaliyoandaliwa kwa ajili ya walimu wakuu na wasimamizi. Madodoso hayo yaliandaliwa ili kukusanya taarifa kuhusu wanafunzi wa Darasa la Pili, walimu wanaofundisha stadi za KKK, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia, madodoso hayo yalilenga kukusanya changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo walimu na wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 1.5 Uchambuzi wa Takwimu na Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Stadi za KKK 2021

Uchambuzi wa takwimu katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulifanyika ili kubaini umahiri wa wanafunzi katika kila stadi. Umahiri huo ulipimwa kwa kuzingatia viwango vya utendaji ambapo alama 0 – 12 ni utendaji hafifu, 13 – 25 utendaji wa wastani, 26 – 37 utendaji mzuri na 38 – 50 utendaji mzuri sana. Utendaji kwa kila stadi umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Utendaji wa Wanafunzi Waliofanya Upimaji Mwaka 2021**

| Stadi | Idadi ya Wanafunzi waliofanya Upimaji | Wanafunzi Waliokuwa na Utendaji wa Wastani hadi Mzuri Sana | |
|---|---|---|---|
| | | **Idadi** | **Asilimia** |
| Kusoma | 27,770 | 18,911 | 68.10 |
| Kuandika | 27,412 | 17,053 | 62.21 |
| Kuhesabu | 27,770 | 16,910 | 60.90 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa wastani wa utendaji kwa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulikuwa ni asilimia 68.10, 62.21 na 60.90 mtawalia. Hii inaonesha kuwa wanafunzi walifanya vizuri zaidi kwenye Stadi za Kusoma.

Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi zilitumika ili kuonesha umahiri wa wanafunzi katika utendaji na changamoto walizokuwa nazo katika kila stadi. Pia, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia jinsi, mahali shule ilipo (kijijini au mjini) na mkoa.

# SURA YA PILI

## UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA

### 2.1 Utangulizi

Lengo la kufanya Upimaji wa Stadi za Kusoma lilikuwa ni kubaini uwezo wa wanafunzi kusoma kifungu cha maneno hamsini kwa ufasaha na kwa kasi inayotakiwa pamoja na kujibu maswali ya ufahamu. Katika upimaji wa Stadi za Kusoma, kila mwanafunzi alipaswa kujibu maswali mawili. Katika swali la kwanza, kipimo cha umahiri wa wanafunzi kilitegemea idadi ya maneno ambayo mwanafunzi aliweza kusoma kwa ufasaha kwa dakika moja. Aidha, katika swali la pili, umahiri wa mwanafunzi ulipimwa kwa kuzingatia uwezo wa kusoma kifungu cha maneno, kuelewa na kutafsiri alichokisoma kisha kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo. Pia, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi umefanyika kwa kuzingatia mikoa, mahali shule ilipo (mijini/vijijini na jinsi (Wavulana/Wasichana).

### 2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi za Kusoma

Katika Upimaji wa Stadi za Kusoma kulikuwa na karatasi mbili ambazo ni karatasi ya mwanafunzi ambayo mwanafunzi alitakiwa kusoma pamoja na fomu maalumu (Skeli ya Upimaji) ambayo mwalimu aliitumia kurekodia alama za mwanafunzi. Karatasi ya mwanafunzi ilikuwa na maswali mawili. Swali la kwanza lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma kifungu chenye maneno hamsini (50) kwa haraka na ufasaha kwa muda wa dakika moja. Swali la pili lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo baada ya kusoma tena kifungu cha maneno. Wakati wa zoezi la upimaji, baadhi ya Halmashauri zilitumia fomu maalum (skeli ya upimaji) kwa ajili ya kurekodia alama za wanafunzi na Halmashauri nyingine zilitumia vishikwambi ambapo alama zilidakwa moja kwa moja.

Upimaji uliofanyika kwa kutumia fomu maalum ya kujaza alama za wanafunzi (skeli ya upimaji) kwa dakika kumi (10) kwa kila mwanafunzi. Dakika moja (1) ilitumiwa na mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha na dakika tatu (3) zilitumika kusoma tena kifungu hicho ili kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo. Aidha, msimamizi alitumia dakika sita (6) kujaza alama za mwanafunzi wakati anasoma, kuuliza maswali ya ufahamu, kukokotoa na kujaza jumla ya alama za mwanafunzi katika skeli ya upimaji.

Vilevile, wanafunzi waliofanya upimaji kwa kutumia kishikwambi walitumia dakika tano kwa kila mmoja. Dakika moja ilitumika kusoma kifungu cha maneno na wakati huo huo msimamizi alirekodi alama za mwanafunzi kwa kutumia mfumo uliokuwa kwenye kishikwambi ambapo alama hizo zilidakwa moja kwa moja. Aidha, dakika tatu zilitumika kusoma tena kifungu cha maneno ili kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo. Kisha, msimamizi alitumia dakika moja kuuliza maswali ya ufahamu.

### 2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi za Kusoma

Viwango vya utendaji vilivyozingatiwa katika upimaji wa Stadi za Kusoma ni utendaji mzuri sana, mzuri, wastani na hafifu. Katika swali la kwanza, mwanafunzi alikuwa na utendaji mzuri sana iwapo alisoma maneno 38-50 kwa usahihi ndani ya dakika moja. Aidha, mwanafunzi aliyesoma maneno 26-37 alikuwa na utendaji mzuri, maneno 13-25, utendaji wa wastani na maneno 0-12 utendaji hafifu.

Wakati wa upimaji, msimamizi alitakiwa kutumia utaratibu ufuatao ili kupata idadi ya maneno yaliyosomwa na mwanafunzi kwa usahihi:

(a) Iwapo mwanafunzi alisoma maneno yote kwa ufasaha, msimamizi aliweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho katika kifungu cha maneno.

(b) Iwapo mwanafunzi alishindwa kusoma neno kwa ufasaha, msimamizi aliweka alama ya mkwaju (/) kwenye neno husika.

(c) Iwapo msimamizi aliweka alama ya mkwaju (/) mwanafunzi alipokosea kusoma neno lakini akarudia kusoma kwa usahihi, alizungushia ile alama ya mkwaju iliyowekwa awali (Ø) katika neno husika.

(d) Iwapo mwanafunzi alishindwa kusoma maneno yote ya sentensi ya kwanza, msimamizi aliweka mkwaju katika maneno hayo. Kisha aliweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho katika sentensi hiyo. Aidha, maneno yote yaliyofuata yalihesabika kuwa ni kosa.

(e) Iwapo mwanafunzi alishindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya dakika moja, msimamizi aliweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho kusomwa na kuhesabia kosa kwa maneno yote yaliyofuata.

Kigezo cha utendaji katika swali la pili kilizingatia idadi ya vipengele vya swali ambavyo mwanafunzi alivijibu kwa usahihi baada ya kusoma kifungu kile kile cha maneno. Swali hilo lilikuwa na vipengele vitano ambavyo mwanafunzi alitakiwa kuvijibu. Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitano alikuwa na utendaji mzuri sana, vinne utendaji mzuri, viwili hadi vitatu utendaji wa wastani na aliyejibu kwa usahihi kipengele kimoja au kushindwa vipengele vyote alikuwa na utendaji hafifu.

## 2.4 Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi za Kusoma

Jumla ya wanafunzi 33,245 walisajiliwa kufanya upimaji wa Stadi ya Kusoma mwaka 2021. Miongoni mwao, wanafunzi 27,770 sawa na asilimia 83.53 walifanyiwa upimaji huo. Wavulana walikuwa 13,619 (49.04%) na wasichana walikuwa 14,151 (50.95%). Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao unaonesha kuwa, asilimia 68.10 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hata hivyo, asilimia 31.90 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu.

### 2.4.1 Swali la 1 : Umahiri wa Kusoma Maneno

Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma maneno hamsini (50) kwa ufasaha kwa dakika moja. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwa kuwa asilimia 66.84 walisoma maneno 13 hadi 50 kwa usahihi. Hata hivyo, wanafunzi wengine (33.16%) walikuwa na utendaji hafifu kwani walisoma maneno 0-12 tu. Jedwali Na. 2 linaonesha utendaji wa wanafunzi katika swali hili.

**Jedwali Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 0 – 12 | Hafifu | 9,208 | 33.16 |
| 13 – 25 | Wastani | 3,179 | 11.45 |
| 26 – 37 | Mzuri | 5,330 | 19.19 |
| 38 – 50 | Mzuri Sana | 10,053 | 36.20 |
| **Jumla** | | **27,770** | **100.00** |

Jumla ya wanafunzi 10,053 (36.20%) waliofanyiwa upimaji wa Stadi za Kusoma walikuwa na utendaji mzuri sana kwa sababu walisoma kwa ufasaha kuanzia maneno 38 hadi 50 kwa dakika moja. Tofauti za utendaji wa wanafunzi hawa zilitegemea kasi na ufasaha katika kusoma maneno. Vielelezo Na. 1 na 2 vinaonesha sampuli za majibu ya wanafunzi ambao walikuwa na utendaji mzuri sana.

Tina na Subira ni marafiki.
Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka[hospitali.]

**Kielelezo Na. 1**: Sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1, mwanafunzi alisoma maneno yote 50 kwa ufasaha ndani ya dakika moja kama msimamizi alivyoonesha kwa kuweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho linalosomeka 'hospitali' kuashiria kuwa mwanafunzi alimaliza kusoma maneno yote.

Tina na Subira ni marafiki.
Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka(hospitali.)

**Kielelezo Na. 2**: Sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika swali la 1

Kielelezo Na. 2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji mzuri sana ingawa alishindwa kusoma kwa ufasaha maneno mawili ambayo ni 'Ng'alo' na 'Kijiji'.

Msimamizi aliweka alama ya mkwaju (/) kwenye maneno ambayo mwanafunzi hakuweza kusoma.

Hata hivyo, asilimia 33.16 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu. Miongoni mwao, wanafunzi 4,154 (14.96%) walisoma neno 1 hadi maneno 12 na wanafunzi 5,054 (18.20%) hawakuweza kusoma hata neno moja katika kifungu cha maneno. Vielelezo Na. 3 na 4 vinaonesha utendaji hafifu.

> Tina na Subira ni marafiki.
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. [Kijiji] chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 3:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 3, mwanafunzi alisoma kwa ufasaha maneno 7 kati ya 10 kwa dakika moja. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alikosa kasi ya usomaji kwani aliishia kusoma neno la kwanza la sentensi ya tatu ambalo ni "kijiji". Hivyo, hakuweza kusoma maneno 40 yaliyofuata.

> Tina na Subira ni [marafiki.]
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 4:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 1

Kielelezo Na. 4 kinaonesha majibu kutoka kwa mwanafunzi ambaye alishindwa kusoma hata neno moja katika kifungu cha maneno. Msimamizi aliweka alama ya mkwaju (/) katika kila neno

na kuweka mabano katika neno la mwisho la sentensi ya kwanza kuashiria kwamba mwanafunzi hakuweza kusoma neno lolote.

Uchambuzi zaidi wa data unaonesha kuwa, asilimia 19.19 ya wanafunzi waliofanya upimaji wa Stadi za Kusoma walikuwa na utendaji mzuri. Walisoma kwa ufasaha kuanzia maneno 26 hadi 37 kwa dakika moja ambayo ni zaidi ya nusu ya maneno yote ambayo walipaswa kusoma katika kifungu cha maneno kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 5.

> Tina na Subira ni marafiki.
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa [amechomwa] na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 5:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji mzuri katika swali la 1

Kielelezo Na. 5 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyesoma kwa ufasaha maneno 36 kati ya 39 kwa dakika moja. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alishindwa kumaliza kusoma maneno 11 yaliyofuata baada ya neno "amechomwa" lililiofungiwa mabano.

Kwa upande mwingine, asilimia 11.45 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani kwani walisoma maneno 13 hadi 25 kwa ufasaha. Kielelezo Na. 6 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji wa wastani.


> Tina na Subira ni marafiki.
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda[kisimani]kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 6:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 6, mwanafunzi alisoma kwa ufasaha maneno 19 kati ya 23 kwa dakika moja. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alikosa kasi ya usomaji kwani alishindwa kumaliza kusoma maneno 27 yaliyofuata baada ya neno “kisimani” lililowekwa kwenye mabano.

### 2.4.2 Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma kila Neno

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kusoma kila neno unaonesha kutofautiana kwa utendaji. Baadhi ya wanafunzi walisoma maneno yote kwa ufasaha na wengine walishindwa kutokana na sababu mbalimbali. Chati Na.1 inaonesha asilimia ya wanafunzi walioweza kusoma kila neno kwa ufasaha.




**Chati Na. 1**: *Utendaji wa wanafunzi katika kusoma kila neno*

Uchambuzi wa takwimu zilizopo katika Chati Na.1 unaonesha kuwa, wanafunzi wengi waliweza kusoma kwa ufasaha maneno yaliyoundwa na silabi moja. Maneno hayo ni: *na* (80.00%), *ni* (79.11%) na *cha* (75.69%). Pia, maneno yaliyoundwa na silabi zenye konsonanti moja na irabu, yalisomwa kwa ufasaha zaidi. Maneno hayo ni pamoja na: *Tina* (74.76%), *kijiji* (72.12%) na *kina* (70.54%).

Aidha, utendaji wa wanafunzi katika kusoma maneno yaliyoundwa na silabi zenye konsonanti mwambatano ulikuwa wa wastani. Maneno hayo yameundwa na silabi zenye mfuatano wa konsonanti na mwanafunzi anatakiwa kutamka kama fungu moja la sauti. Hivyo, ilisababisha changamoto kwa baadhi ya wanafunzi kutamka kama fungu moja la sauti ilihali yanaonekana maumbo mawili ya sauti. Maneno yenye silabi mwambatano yaliyokuwa na utendaji wa wastani yalikuwa kama ifuatavyo: shida (61.47%), kubwa (58.52%), walikwenda (52.97), alichukua (51.04%), ndoo (51.47%) na akaanza (46.39%).

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kusoma kwa ufasaha maneno kama vile: *Subira* (45.05%), *Mara* (56.00%) na *Ng'alo* (69.63%). Wanafunzi hao walishindwa kusoma maneno hayo kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mfano, neno 'Ng'alo' lililoundwa na sauti ya king'ong'o (*ng*') ambayo hutamkwa kwa kutoa hewa kwa njia ya pua, wanafunzi walio wengi walitamka sauti hiyo kwa kutoa hewa kwa njia ya mdomo. Hivyo, walitamka *Ngalo* badala ya *Ng'alo*.

Vilevile, wanafunzi wengine walishindwa kusoma neno 'Mara' na 'Subira' kutokana na athari za lugha za makabila (Lugha mama) katika lugha ya pili ambayo ni Kiswahili. Hii inatokana na kutokuwepo kwa baadhi ya sauti katika lugha za makabila zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, kutokuwepo kwa sauti 'r' katika baadhi ya lugha za makabila kulisababisha baadhi ya wanafunzi wa makabila hayo kushindwa kutamka sauti 'r' badala yake walitamka 'l'. Hivyo, neno 'Subira' walitamka 'Subila' na neno 'Mara' walitamka 'Mala'.

Pia, sauti 'r' na 'l' ni sauti zilisababisha changamoto kwa wanafunzi kutokana na namna ya utamkaji na mahali pa matamshi. Sauti hizi hutamkwa kwenye ukingo wa ufizi na

kuwepo kwa kizuizi sehemu ya hewa. Sauti hizo hujulikana kama vilainisho/vimiminiko. Sauti ‘r’ inapotamkwa ncha ya ulimi hugusana na sehemu ya nyuma ya ufizi wakati huo pembe za ulimi hugusana na kingo za kaakaa. Sauti ‘l’ inapotamkwa, ncha ya ulimi huinuliwa na kugusana na kingo na ufizi na kusababisha hewa kupita kwenye pembe za ulimi. Hii ilikuwa changamoto kwa baadhi ya wanafunzi kutofautisha namna ya kutamka sauti hizo. Kwa hiyo, baadhi ya wanafunzi walitamka sauti ‘r’ kama ‘l’ kwa mfano katika maneno: *Subila*, *Mala* na *lafiki* badala ya *Subira*, *Mara* na *rafiki* mtawalia. Pia, wanafunzi wengine walitamka ‘l’ kama ‘r’ mfano: *kerere* na *Ng’aro* badala ya *kelele* na *Ng’alo* mtawalia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 24,064 sawa na asilimia 86.65 walishindwa kumaliza kusoma kwa ufasaha kifungu cha maneno hamsini ndani ya muda wa dakika moja. Hii inamaanisha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na uwezo wa kusoma kwa kasi. Wengi wao waliishia kusoma neno la *thelathini na sita* ambalo ni ‘kelele’. Maneno mengine waliyoshindwa kusoma ndani ya muda uliopangwa ni : *kumbe* (57.57%), *alikuwa* (58.71%), *amechomwa* (66.99%), *na* (60.01 %), *mwiba* (65.42%), *Hatimaye* (70.45%), *Subira* (74.77%), *alishindwa* (76.36%), *kubeba (72.54%), ndoo* (74.54%), *wazazi* (75.62%), wake (76.26%), *walimpeleka (81.21%)* na *Hospitali* (82.04%). Hata hivyo, uwezo wa kusoma wa wanafunzi wengi ulikuwa juu ya wastani kwani walisoma kwa ufasaha maneno ishirini na saba (27) kwa dakika.

### 2.4.3 Swali la 2 : Umahiri wa Ufahamu wa Kusoma na Kusikiliza

Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma kifungu cha maneno, kukielewa na kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho kwa mdomo. Swali lilikuwa na vipengele vitano ambavyo vilitokana na kifungu cha maneno ambacho kilitakiwa kusomwa kwa muda wa dakika tatu. Kifuatacho ni kifungu cha maneno alichotakiwa kusoma mwanafunzi na kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo.

*Tina na Subira ni marafiki.*
*Wanaishi kijiji cha Ng’alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda*

*kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.*

Kwa ujumla, utendaji wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwani wanafunzi wengi (60.03%) walijibu kwa usahihi vipengele viwili hadi vitano vya swali. Jedwali Na. 3 linaonesha utendaji wa wanafunzi katika swali la hili.

**Jedwali Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali ya Ufahamu**

| Idadi ya Vipengele | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 0-1 | Hafifu | 11,099 | 39.97 |
| 2-3 | Wastani | 5,767 | 20.77 |
| 4 | Mzuri | 7,292 | 26.26 |
| 5 | Mzuri sana | 3,612 | 13.01 |
| **Jumla** | | **27,770** | **100.00** |

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 11,099 (39.97%) walikuwa na utendaji hafifuambapo wanafunzi 3,849 (13.86%) walijibu kwa usahihi kipengele kimoja tu kati ya vitano. Aidha, wanafunzi 7,250 (26.11%) hawakuweza kujibu kipengele hata kimoja kati ya vyote vitano. Vielelezo Na. 7 na 8 vinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji hafifumtawalia.

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |

**Kielelezo Na. 7:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 7, mwanafunzi alijibu kwa usahihi kipengele kimoja tu kati ya vitano kwa kuwa alishindwa kusoma kwa ufasaha kifungu cha maneno na kukielewa. Hivyo, alishindwa kukumbuka maudhui yaliyokuwemo katika kifungu hicho.

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |

**Kielelezo Na. 8:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji hafifu katika swali la 2

Kielelezo Na. 8 kinaonesha majibu kutoka kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi kipengele chochote na kusababisha kuwa na utendaji hafifu.

Hata hivyo, wanafunzi 7,292 (26.26%) walikuwa na utendaji mzuri kwa kuwa walijibu vipengele vinne vya swali kwa usahihi. Hii ni kwa sababu walikuwa na uwezo mkubwa wa kusoma kwa ufahamu ambao uliwawezesha kukumbuka maudhui ya kifungu

cha maneno walichokisoma. Kielelezo Na. 9 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata utendaji mzuri.

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |

**Kielelezo Na. 9:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji mzuri katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 9, mwanafunzi alijibu vipengele vinne kwa usahihi. Hii inadhihirisha kuwa alielewa kifungu cha maneno hivyo akajibu maswali yaliyopima ngazi za chini na za juu za kufikiri.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 5,767 sawa na asilimia 20.77 walijibu vipengele viwili hadi vitatu vya swali kwa usahihi. Hii inadhihirisha kwamba wanafunzi hao walikuwa na utendaji wa wastani katika kusoma na kuelewa kifungu cha maneno. Kielelezo Na. 10 kinaonesha sampuli ya mwanafunzi mwenye utendaji wa wastani.

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |

**Kielelezo Na. 10:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 10, mwanafunzi alijibu kwa usahihi vipengele vitatu vya swali. Hii inaonesha kuwa mwanafunzi huyu alikuwa na utendaji wa wastani katika kujibu maswali ya ufahamu. Aidha, aliweza kujibu kwa usahihi kipengele cha 5 kilichopima umahiri wa ngazi ya juu zaidi ya kufikiri.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 3,612 (13.01%) walijibu vipengele vyote vitano kwa usahihi jambo linaloonesha utendaji mzuri sana. Wanafunzi wa kundi hili walikuwa na uwezo wa kusoma, kuelewa na kutafsiri kile walichosoma. Hii iliwawezesha kujibu kwa usahihi maswali yaliyopima ngazi ya kukumbuka na kutathmini. Kielelezo Na.11 kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mmoja wa wanafunzi.


| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |

**Kielelezo Na. 11:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji mzuri sana katika swali la 2

Kielelezo Na. 11 kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mwanafunzi ambaye alijibu kwa usahihi vipengele vitano katika swali la 2. Majibu hayo yanaonesha kuwa wanafunzi wa kundi hili walikuwa na stadi za kutosha za ufahamu.

### 2.4.4 Utendaji wa Wanafunzi katika kila Kipengele cha Ufahamu

Utendaji wa wanafunzi katika kujibu vipengele vya swali hili ulitofautiana kutokana na sababu mbalimbali. Pamoja na majibu tofauti yaliyotolewa na wanafunzi, kwa wastani wanafunzi wote walijibu kwa usahihi vipengele viwili vya swali. Hivyo, uwezo wa wanafunzi wa kusoma, kuelewa na kujibu maswali ulikuwa wa wastani. Chati Na. 2 inaonesha asilimia ya utendaji wa wanafunzi katika kila kipengele.




**Chati Na. 2**: *Utendaji wa wanafunzi katika kila kipengele cha swali la 2*

Jumla ya wanafunzi 16,654 (59.97%) walijibu kwa usahihi kipengele cha kwanza kilichouliza "Rafiki yake Tina anaitwa nani?" Wanafunzi hawa walijibu kwa usahihi kipengele hiki kwa sababu walisoma kifungu cha maneno kwa ufasaha na kuelewa maudhui yake. Kwa hiyo, walikumbuka jina la rafiki yake Tina kuwa ni Subira.

Vilevile, wanafunzi 14,606 sawa na asilimia 52.60 walijibu kwa usahihi kipengele cha tano cha swali kilichouliza "Kwa nini Subira alipelekwa hospitali?" Ingawa kipengele hiki kilipima kiwango cha juu cha kufikiri, kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi wengi. Hii inadhihirisha kwamba wanafunzi hao walielewa kifungu cha maneno. Baadhi ya wanafunzi walihusisha swali na uzoefu wa maisha ya kila siku kwamba mtu anayepelekwa hospitali ni mgonjwa au aliyeumia hivyo, anahitaji matibabu.

Katika kipengele cha tatu, wanafunzi waliulizwa 'Tina na Subira walikwenda wapi?' Utendaji wa wanafunzi katika kipengele hiki ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 13,898 (50.05%) walijibu kwamba 'walikwenda kisimani'. Majibu hayo yanaashiria kuwa walikuwa na umahiri wa kusoma kwa ufasaha na kuelewa mawazo makuu ya kifungu cha maneno walichosoma. Hivyo, walijibu kwa usahihi mahali ambapo Tina na Subira walikokwenda kuwa ni 'Kisimani'.

Hata hivyo, kipengele cha pili kilichouliza “Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi wachache (34.97%). Jibu sahihi katika kipengele hiki ni “Ng’alo”. Wanafunzi wengi (65.03%) walishindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa sababu walishindwa kutamka kwa ufasaha neno “Ng’alo” lenye sauti ya king'ong'o (ng’), badala yake walitamka kama sauti ya mdomoni “Ng” hivyo wakatamka ‘Ngalo’.

Aidha, kipengele cha nne kilichouliza “Subira alitumia nini kujaza ndoo yake?” kilikuwa na utendaji hafifukwani ni asilimia 37.11 tu ya wanafunzi ndio walijibu kipengele hiki kwa usahihi. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa asilimia ya wanafunzi wengi (62.89%) walishindwa kubainisha kuwa chombo maalumu alichotumia Subira kuteka maji ndani ya kisima kinaitwa ‘kata’. Baadhi ya wanafunzi walitoa majibu yasiyo sahihi kama vile: *ndoo*, *kikombe*, *pipa* na *chungu* ambavyo ni vyombo vinavyotumika kuhifadhi maji lakini sio kisimani. Hata hivyo, vyombo hivi havikutajwa katika kifungu cha maneno. Majibu haya yanaonesha kuwa, wanafunzi hao hawakuelewa swali hivyo walitoa majibu kulingana na uzoefu wao wa maisha ya kila siku.


## 2.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo na Jinsi

Katika upimaji wa Stadi ya Kusoma, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia mikoa, mahali shule ilipo (mijini au vijijini), na jinsi (Wavulana na Wasichana). Lengo la ulinganifu huu lilikuwa kubainisha tofauti za utendaji wa wanafunzi katika makundi hayo ili kutoa mapendekezo yenye tija yanayolenga kuboresha mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa kwa Mwaka 2019 na 2021

Upimaji wa Stadi za Kusoma kwa mwaka 2021 ulifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara kama ulivyofanyika mwaka 2019. Utendaji wa wanafunzi kimkoa ulilinganishwa kati ya mwaka 2019 na 2021 ili kubaini kama kuna ongezeko au kupungua kwa uwezo wa kusoma wa wanafunzi kimkoa. Katika kufanya ulinganifu huo, vigezo vifuatavyo vimezingatiwa: mwanafunzi aliyepata alama 0-

12 alihesabika kuwa na utendaji hafifu, 13-25 wastani, 26-37 utendaji mzuri na 38-50 utendaji mzuri sana. Chati Na. 3 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kimikoa.




**Chati Na. 3:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kimkoa*

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kimkoa katika upimaji wa mwaka 2019 na 2021 unaonesha kuwa utendaji wa kitaifa mwaka 2021 umeshuka kwa asilimia 6.70. Mwaka 2019 ufaulu wa kitaifa ulikuwa asilimia 74.80 wakati mwaka 2021 ulishuka hadi asilimia


68.10. Mkoa wa Dar es Saalam uliongoza kwa ufaulu kwa miaka yote miwili ingawa utendaji wake ulishuka kwa asilimia 3.17 kutoka asilimia 92.40 mwaka 2019 hadi asilimia 89.23 mwaka 2021.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa kuna mikoa mitano ambayo utendaji wake ulipanda kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na mwaka 2019. Asilimia ya utendaji wa wanafunzi katika mikoa hiyo iliongezeka kama ifuatavyo: Kilimanjaro (3.40%), Arusha (4.10%), Kagera (6.01%), Songwe (1.25%) na Mwanza (0.79%).

Kwa upande mwingine, mkoa wa Katavi haukufanya vizuri mwaka 2021 ikilinganishwa na mwaka 2019. Kiwango chake cha utendaji kilishuka kwa asilimia 17.53 kutoka asilimia 63.60 mwaka 2019 hadi asilimia 46.07 mwaka 2021. Hivyo, mkoa wa Katavi ulikuwa na utendaji wa chini kuliko mikoa yote Tanzania Bara.

### 2.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo

Idadi ya wanafunzi waliofanyiwa upimaji wa Stadi za Kusoma mwaka 2021 ilikuwa 27,770. Kati yao, wanafunzi 13,834 (49.82%) walitoka shule za mjini na wanafunzi 13,936 (50.18%) walitoka shule za vijijini. Uchambuzi unaonesha tofauti katika utendaji wao kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.





**Chati Na. 4:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kati ya shule za mjini na vijijini*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa wanafunzi waliotoka katika shule za mjini walikuwa na utendaji mzuri huku utendaji wa wanafunzi wa shule za vijijini ukiwa ni asilimia 62.61. Kwa hiyo, wanafunzi kutoka katika shule za mjini walifanya vizuri zaidi kwa asilimia 11.01 ikilinganishwa na wanafunzi wa shule za vijijini kama ilivyokuwa katika upimaji uliofanyika mwaka 2019 ambapo wanafunzi wa shule za mjini walifanya vizuri zaidi kwa asilimia 6.14.

### 2.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi

Jumla ya wanafunzi 27,770 walifanyiwa upimaji wa Stadi za Kusoma mwaka 2021 ambapo wasichana walikuwa 14,151 (50.95%) na wavulana 13,619 (49.04%). Uchambuzi wa data ulifanywa ili kubaini tofauti ya utendaji kati ya wavulana na wasichana na muhtasari wa ulinganifu umebainishwa katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ulinganifu wa utendaji kati ya wavulana na wasichana*

Katika Chati Na. 5, wasichana waliopata utendaji wa wastani hadi vizuri sana ni asilimia 72.33 huku wa wavulana ukiwa asilimia 63.70. Hivyo, utendaji wa wasichana ulikuwa mzuri zaidi kuliko wa wavulana.

## 2.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi za Kusoma

Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi katika upimaji wa Stadi za Kusoma unaonesha kuwa wanafunzi walipata utendaji wa wastani asilimia 68.10. Wanafunzi hao walisoma maneno 13 mpaka 50 kwa ufasaha kwa dakika moja na kujibu maswali 2 hadi 5 ya ufahamu kwa usahihi. Kwa upande mwingine, asilimia 31.90 ya wanafunzi walipata utendaji hafifukwa kuwa walishindwa kusoma maneno mengi kwa ufasaha. Kwa mfano, walishindwa kusoma maneno yaliyoundwa kwa mfuatano wa konsonanti kama vile ‘kubwa’, ‘walikwenda’, ‘alichukua’, ‘ndoo’ na ‘akaanza’, maneno yaliyoundwa na sauti ‘r’ kama vile ‘Subira’ na ‘Mara’ na neno lililokuwa na sauti ya king’ong’o (ng’) ambalo ni “Ng’alo”.

# SURA YA TATU

# UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua Stadi za Kuandika kwa kuzingatia muundo wa karatasi ya upimaji, vigezo vya kupima umahiri wa wanafunzi na uchambuzi wa takwimu na majibu ya wanafunzi. Vilevile, sura hii inaeleza maeneo ambayo wanafunzi walifikia viwango vya utendaji kama vile, vizuri sana (alama 38 hadi 50), vizuri (alama 26 hadi 37) wastani (alama 13 hadi 25) na hafifu (alama 0 hadi 12). Aidha, sura hii inaonesha matokeo kuhusu uwezo wa wanafunzi kutambua na kuandika majina ya picha kwa usahihi, kuandika maneno kwa herufi kubwa na kunakili kifungu cha maneno kisha kutumia alama za uandishi kwa usahihi. Vilevile, sura hii inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kuandika kwa kuzingatia mikoa, mahali shule ilipo (mijini/vijijini) na jinsi (wavulana/wasichana).

## 3.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi za Kuandika

Karatasi ya upimaji ya Stadi za Kuandika ilikuwa na maswali matatu (3). Swali la kwanza (1) lilikuwa na vipengele kumi (10). Mwanafunzi alitakiwa kutambua na kuandika jina la picha. Swali la pili mwanafunzi alitakiwa kuandika maneno kumi (10) aliyopewa kwa herufi kubwa na swali la tatu lilimtaka mwanafunzi kunakili kifungu cha maneno alichopewa na kuweka alama sahihi za uandishi. Lengo la upimaji lilikuwa ni kubaini uwezo wa mwanafunzi wa kumudu Stadi za kuandika.

## 3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi za Kuandika

Umahiri wa mwanafunzi katika Stadi za Kuandika ulipimwa kwa kuzingatia viwango vinne (4) vya utendaji ambavyo ni : hafifu, wastani, mzuri na mzuri sana. Katika swali la 1 na la 2 umahiri wa mwanafunzi ulikuwa hafifu endapo aliandika kwa usahihi vipengele 0 - 2, wastani vipengele 3 - 5, mzuri vipengele 6 - 8 na mzuri sana vipengele 9 – 10. Umahiri wa mwanafunzi katika kuandika herufi kubwa ulizingatia uwezo wake katika kuumba herufi kubwa. Aidha, katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi, umahiri wa mwanafunzi ulizingatia jumla ya alama alizopata baada ya kunakili kifungu cha maneno na kutumia alama sahihi za uandishi. Iwapo mwanafunzi alipata

alama 0 – 5 baada ya kunakili maneno na kuweka alama za uandishi ilihesabika ni utendaji hafifu, wastani alama 6 – 10, mzuri 11 – 15 na mzuri sana alama 16 – 20.

### 3.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Stadi za Kuandika

Takwimu za majibu ya wanafunzi zinaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 27,412 (100%) walifanya upimaji katika Stadi za Kuandika. Miongoni mwao, asilimia 62.21 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha, asilimia 37.79 walikuwa na utendaji hafifu. Jedwali Na. 4 linaonesha utendaji wa jumla katika Stadi za Kuandika.

**Jedwali Na. 4: Utendaji wa Jumla wa Wanafunzi katika Stadi za Kuandika**


| Umahiri Uliopimwa | Viwango vya Utendaji | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu | | Wastani | | Mzuri | | Mzuri Sana | |
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Kuunda Maneno | 7,982 | 29.12 | 4,314 | 15.74 | 10,642 | 38.82 | 4,474 | 16.32 |
| Kuandika Herufi Kubwa | 17,637 | 64.34 | 2,824 | 10.30 | 2,974 | 10.85 | 3,977 | 14.51 |
| Kunakili Kifungu cha Maneno na kuweka Alama Sahihi za Uandishi | 15,958 | 58.22 | 1,772 | 6.46 | 4,409 | 16.08 | 5,273 | 19.24 |

Jedwali Na. 4 linaonesha wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha, katika umahiri wa kuandika majina ya picha, utendaji ulikuwa ni asilimia 70.88, kuandika herufi kubwa asilimia 35.66 na kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi ulikuwa asilimia 41.78.

#### 3.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kutambua na Kuandika Jina la Picha Husika

Katika uchambuzi wa kutambua majina ya picha na kuunda maneno kwa usahihi ilibainika kuwa, wanafunzi 19,430 (70.88%)

walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana na wanafunzi 7,982 sawa na asilimia 29.12 walikuwa na utendaji hafifukama inavyoonekana katika Chati Na. 6.






**Chati Na. 6**: *Utendaji wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha*

Chati Na. 1 inaonesha viwango vya utendaji vya wanafunzi kwa swali la 1. Aidha, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa sababu wanafunzi waliweza kutambua picha na kuumba herufi za majina ya picha hizo kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 7,982 (29.12%) walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kutambua picha na kuandika kwa usahihi majina yanayowakilisha picha hizo. Baadhi yao walichanganya herufi kubwa na ndogo katika kuunda maneno. Pia, wanafunzi wengine waliandika baadhi ya majina kwa kukosea herufi (tahajia), wengine walinakili maelezo ya swali. Wengine waliandika majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali na miongoni mwao wapo walioshindwa kuandika majina ya picha zenye silabi za herufi mwambatano. Kielelezo Na. 12 kinaonesha sampuli za majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji hafifu.

. **Andika** majina ya **picha** hizi :

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) |  DEgE | (b) |  gauni |
| (c) |  Basikari | (d) |  siba |
| (e) |  chanuo | (f) |  mune |






**Kielelezo Na. 12**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi

Katika Kielelezo Na. 12, mwanafunzi alishindwa kuandika majina ya picha zenye silabi mwambatano kama vile; “Ndege” aliandika “Dege”, “Simba” aliandika “Siba”, “Kitanda” aliandika “kitada”, “Jembe” aliandika “Jenbe” na “Pundamilia” aliandika “pondamiraa”. Aidha, mwanafunzi huyo aliweza kuandika kwa usahihi neno “gauni” katika kipengele (b) na neno “chanuo” katika kipengele (e) na hivyo kupata alama za kiwango kisichoridhisha.

Aidha, wanafunzi 4,314 (15.74%) walikuwa na utendaji wa wastani. Wanafunzi hao waliweza kutambua picha za vipengele vitatu hadi vitano na kuandika majina ya picha hizo kwa usahihi na kupata alama 6 hadi 10. Hata hivyo, wengine waliandika baadhi ya majina kwa lugha za asili na wengine walishindwa kuandika maneno yanayoundwa na konsonanti ambayo ni nazali. Kielelezo Na. 13 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.

1. **Andika** majina ya **picha** hizi :

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) |  Denge | (b) |  gonDi |
| (c) |  jilushe | (d) |  Simba |
| (e) |  chanuo | (f) |  mukono |






**Kielelezo Na. 13**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani

Katika Kielelezo Na. 13, mwanafunzi aliweza kuandika majina sahihi katika kipengele (d), (e), na (i). Aidha, alishindwa kuandika majina sahihi katika kipengele (a), (b), (c), (h), (f), (g) na (j). Katika kipengele (a) na (f), mwanafunzi alishindwa kuandika kwa usahihi majina yanayoanza na konsonanti, ambayo ni nazali “n” na “m” hivyo kuandika “Denge” badala ya *Ndege* na “Mukono” badala ya *mkono* mtawalia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 10,642 (38.82%) walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi hao walitambua baadhi ya picha na kuandika majina ya picha hizo kwa usahihi (majina 6 hadi 8) na kupata alama 12 hadi 16. Kielelezo Na. 14 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.

1. **Andika** majina ya **picha** hizi :

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) |  ndege | (b) |  gauni |
| (c) |  basikeli | (d) |  Simba |
| (e) |  kichanio | (f) |  mukono |





**Kielelezo Na. 14**: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri

Katika Kielelezo Na. 14 mwanafunzi aliweza kuandika majina sahihi katika vipengele vinane (8) na hivyo kuwa na utendaji mzuri. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alishindwa kuandika majina sahihi katika vipengele (c) na (f).

Aidha, wanafunzi 4,474 (16.32%) waliokuwa na utendaji mzuri sana, walitambua picha zote kumi (10) na kuandika majina ya picha hizo kwa usahihi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 15.

1. **Andika** majina ya **picha** hizi :

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) |  Ndege | (b) |  Gauni |
| (c) |  Baiskeli | (d) |  Simba |
| (e) |  Chanuo | (f) |  Mkono |




**Kielelezo Na. 15**: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana

Katika Kielelezo Na. 15 mwanafunzi aliweza kuandika majina ya picha za vipengele vyote kumi (a - j) kwa usahihi na hivyo kuwa na utendaji mzuri sana.

### 3.4.2 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi katika kila Neno

Uchambuzi wa takwimu ulifanyika ili kubainisha utendaji wa wanafunzi katika kila neno lililopimwa. Utendaji wao katika kila neno ulikuwa kama ifuatavyo:

#### (a) Ndege

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 15,441 (56.33%) waliandika kwa usahihi jina “ndege”. Wanafunzi hao

walikuwa na umahiri wa kutambua picha na kuhusianisha na jina sahihi linalowakilisha picha husika kisha kuandika jina husika kwa kuumba herufi zote kwa usahihi.

Hata hivyo, wanafunzi 11,971 (43.67%) walishindwa kutambua picha na kuandika jina sahihi. Wapo waliofananisha na “garimoshi”, wengine waliandika “nyumba” na wengine waliandika “samaki” majibu ambayo siyo sahihi.

**(b) Gauni**

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 17,736 (64.70%) waliweza kutambua picha husika na kuandika jina lake “gauni” kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuandika maneno yenye silabi zilizoundwa na konsonanti na irabu.

Aidha, wanafunzi 9,676 (35.30%) walishindwa kuandika jina “gauni” kwa usahihi. Baadhi yao waliandika majina yanayohusiana na picha hiyo kimuonekano kama vile, “kanzu” na “gunia”, wengine waliandika “pazia” na wengine waliandika “mdoli”. Majibu ambayo yalikuwa tofauti na matakwa ya swali.

**(c) Baiskeli**

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 21,774 (79.43%) walitambua picha ila walishindwa kuandika jina la picha husika “baiskeli” kwa usahihi kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maneno yanayoundwa na silabi nne, ambazo ni /ba/ /i/ /ske/ /li/ ambapo silabi mbili kati ya hizo zinaundwa na konsonanti irabu ambazo ni /ba/ na /li/ na silabi /i/ inaundwa na irabu pekee. Aidha, silabi /ske/ huundwa na konsonanti konsonanti irabu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 5,638 (20.57%) waliweza kutambua picha na kuandika jina kwa usahihi, kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maneno yanayoundwa na silabi nne (4), ambazo ni /ba/ /i/ /ske/ /li/

hivyo kuweza kuelewa silabi zinazoundwa na konsonanti irabu pamoja na konsonanti konsonanti irabu.

**(d) Simba**

Wanafunzi 17,457 (63.68%) waliweza kuandika jina "simba" kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutambua picha kwa sababu ni aina ya mnyama anayejulikana na picha zake zinapatikana katika mazingira mbalimbali kama vile, shuleni, nyumbani na sehemu za maonesho. Aidha, neno *simba* limeundwa na silabi mbili ambazo ni /si/ na /mba/ ambapo ni rahisi kwa mwanafunzi kuandika maneno yanayoundwa na silabi mbili kuliko silabi zaidi ya mbili.

Hata hivyo, wanafunzi 9,955 (36.32%) walishindwa kuandika jina "simba" kwa usahihi. Baadhi yao waliandika maneno "thimba", "siba" "shimba", kutokana na kuathiriwa na lugha mama ambapo, walishindwa kutofautisha sauti "s", na "th", kutokana na matamshi ya sauti hizo kuwa na sifa moja ya utamkwaji ambayo ni vikwamizi. Wanafunzi wengine walikuwa na changamoto katika kuandika sauti zenye silabi zenye herufi mwambatano /mba/.

**(e) Chanuo**

Uchambuzi katika kipengele hiki unaonesha kuwa wanafunzi 16,646 (60.73%) walishindwa kuandika jina "chanuo" ambapo miongoni mwao waliandika *kitana, kichaniu, chanulo* na *chanuwo*. Wanafunzi hao walitambua picha kwa sababu majina hayo hutumika katika mazingira yao ila waliandika majina yasiyo sahihi.

Aidha, wanafunzi 10,766 (39.27%) waliweza kutambua picha husika na kuandika kwa usahihi neno "chanuo". Waliweza kubaini kuwa neno hilo limeundwa na silabi tatu /cha/ /nu/ /o/ hivyo kuliandika kwa usahihi kwa kuzingatia misingi ya uundaji wa maneno.

**(f) Mkono**

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 15,610 (56.95%) walikuwa na utendaji mzuri kwani waliweza kutambua picha husika na kuandika jina kwa usahihi "mkono". Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuhusisha picha na kuumba herufi zinazounda neno "mkono". Aidha, neno hilo ni rahisi kwa kuwa limeundwa na silabi ambazo ni konsonanti na irabu na konsonanti pekee.

Aidha, wanafunzi 11,802 (43.05%) hawakuweza kuandika neno "mkono" kwa usahihi kwa kuwa hawakuwa na umahiri wa kuunda herufi za neno hilo. Hivyo, waliandika maneno yasiyo sahihi kama "vidole", "kono" "kibao", "jani" na "mti". Aidha, waliandika majina hayo kwa kuhusianisha na picha husika.

**(g) Kitanda**

Katika kipengele hiki wanafunzi 16,069 (58.62%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "kitanda". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha waliyopewa na kuandika jina la picha hiyo kwa usahihi. Aidha, jina hilo limeundwa na silabi tatu zenye muundo wa konsonanti irabu na konsonanti konsonanti irabu ambao ni muundo rahisi kwa wanafunzi kuunda neno. Vilevile, "kitanda" ni kifaa ambacho wanafunzi walio wengi wanakitumia kila siku katika mazingira yao ya nyumbani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 11,343 (41.38%) hawakuandika jina kwa usahihi kwa sababu hawakuwa na umahiri wa kuhusianisha picha na jina husika. Baadhi yao waliandika maneno yasiyohusiana na picha hiyo, kama vile, neno "kitada". Wanafunzi hao walikuwa na changamoto ya uandishi wa sauti za nazali /n/ wengine waliandika "tanda" na kupata utendaji hafifu.

**(h) Kiatu**

Jumla ya wanafunzi 14,902 (54.36%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "kiatu". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha husika na kuhusianisha na herufi za neno, kisha kuandika kwa usahihi. Aidha, wanafunzi hawa walikuwa na umahiri katika kuunda maneno yenye silabi tatu zinazoundwa na konsonanti irabu pamoja na irabu pekee.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 12,510 (45.64%) walikuwa na utendaji hafifukatika kuunda neno “kiatu” kwa sababu hawakuwa na umahiri wa kuhusianisha picha na jina husika. Walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina silabi tatu ambazo ni /ki/ /a/ /tu/ zenye muundo wa konsonanti irabu na irabu pekee. Aidha, baadhi ya wanafunzi waliathiriwa na lugha zao za asili (lugha mama) na kuandika *fiatu* na *kilatu.*

**(i) Jembe**

Uchambuzi wa upimaji unaonesha kuwa wanafunzi 16,593 (60.53%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina “jembe”. Wanafunzi hao waliweza kutambua picha husika na kisha kuandika jina linalohusiana na picha hiyo kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi 10,819 (39.47%) hawakuweza kutambua jina linalohusiana na picha hiyo. Wanafunzi hao waliandika majina kama vile “gembe”, “leki”, “mpini’ na “mti”. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha “jembe” na “mpini” ingawa jembe hushikiliwa na mpini. Aidha, wengine walishindwa kutokana na kukosa umahiri wa kuunda maneno yenye herufi mwambatano “mb” hivyo kuandika “jenbe” badala ya “Jembe”.

**(j) Pundamilia**

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, wanafunzi 18,462 (67.35%) hawakuwa na umahiri wa kutosha katika kuandika jina "pundamilia." Wanafunzi hao waliandika


majina kama vile *nyau, mbwa, chui.* Wengine waliandika *pudamilia* na wengine *pundamiliya*. Aidha, wanafunzi hao, wana changamoto ya uandishi wa sauti za nazali /n/ na kuongeza herufi –y- katika neno *pundamiliya.* Wengine walishindwa kutokana na kukosa umahiri wa kuunda neno lenye silabi tano (5) ambazo ni /pu/ /nda/ /mi/ /li/ /a/.

Hata hivyo, wanafunzi 8,950 (32.65%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina lililowakilishwa na picha husika kwa sababu waliweza kuandika jina "pundamilia" kwa usahihi. Wanafunzi hao waliweza kuunda neno lenye silabi tano (5) zenye mchanganyiko wa sauti za konsonanti na irabu.

### 3.4.3 Swali la 2 : Kuandika Maneno kwa Herufi Kubwa

Swali hili lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kuandika herufi kubwa na lilikuwa na alama 10.

Jumla ya wanafunzi 27,412 (100%) walijibu swali hili na lilikuwa na ufaulu wa wastani. Chati Na. 2 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na. 7:** *Utendaji wa wanafunzi katika kuandika maneno kwa herufi kubwa*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa wanafunzi 3,977 (14.51%) walikuwa na utendaji mzuri sana kwa kuwa waliweza kuandika kwa herufi

kubwa maneno 9 hadi 10 kwa usahihi. Wanafunzi 2,974, (10.85%) walikuwa na utendaji mzuri kwa kuweza kuandika kwa herufi kubwa maneno 6 hadi 8 kwa usahihi. Aidha, wanafunzi 2,824 (10.30%) walikuwa na utendaji wa wastani kwa kuweza kuandika maneno 3 hadi 5. Vilevile, wanafunzi 17,637 (64.34%) walikuwa na utendaji hafifu kwa kuandika kwa herufi kubwa maneno 0 hadi 2 kwa usahihi.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 17,637 (64.34%) walikuwa na kiwango hafifu cha utendaji kwa kuwa walishindwa kuandika maneno kwa herufi kubwa. Kati yao, walichanganya herufi kubwa na ndogo katika kuunda neno. Wengine waliandika herufi ya kwanza kwa kila neno walilopewa badala ya kuandika neno kamili kwa herufi kubwa. Aidha, wanafunzi wengine walitunga sentensi badala ya kuandika maneno kwa herufi kubwa. Wengine waliandika majina ya picha ya swali la kwanza badala ya kuandika kwa herufi kubwa maneno waliyopewa. Kielelezo Na. 16 (a - c) ni sampuli za majibu ya wanafunzi waliokuwa na kiwango cha utendaji kisichoridhisha.

2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.

(a) juisi ____j____

(b) maji ____M____

(c) asha ____A____

(d) faida ____F____

(e) gurudumu ____G____

(f) papai ____P____


(g) zabibu ____Z____

(h) dodoma ____D____

(i) nanasi ____N____

(j) mwanza ____Mw____


**Kielelezo Na. 16 (a)**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika herufi ya kwanza kwa kila neno alilopewa



2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.

| | | |
|---|---|---|
| (a) | juisi | JuiSi |
| (b) | maji | MAJI |
| (c) | asha | aSha anakula |
| (d) | faida | anaLima Shambani |
| (e) | gurudumu | anachunga ng'ombe |
| (f) | papai | popo anakula Lote |
| (g) | zabibu | tunakula na Shangazi |
| (h) | dodoma | tunakula na bibi |
| (i) | nanasi | |
| (j) | mwanza | niko ShuLeni ninaSoma |

**Kielelezo Na. 16 (b):** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyetunga sentensi kwenye baadhi ya majibu yake badala ya kuandika maneno aliyopewa kwa herufi kubwa. Hata hivyo, alipata kipengele cha (a) na (b). Kipengele (i) hakujaza kabisa na kupata alama hafifu



2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.


(a) juisi NDEG
(b) maji GUNI
(c) asha BISKELI
(d) faida SIMA
(e) gurudumu CRANIO
(f) papai KITANDA
(g) zabibu KIATU
(h) dodoma SROKa
(i) nanasi puNDALIA
(j) mwanza ______

**Kielelezo Na. 16 (c)**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika baadhi ya majina ya picha katika swali la kwanza badala ya kuandika majina husika kwa herufi kubwa. Mwanafunzi pia alishindwa kujibu kipengele (j) na hivyo kupata alama za hafifu

Kielelezo Na. 16 (a), (b) na (c) ni sampuli za majibu ya wanafunzi wenye utendaji hafifu katika kuandika maneno kwa herufi kubwa. Hivyo, kujibu kinyume na matakwa ya swali, na kupata alama za kiwango kisichoridhisha.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 2,824 (10.30%) walikuwa na utendaji wa wastani. Wanafunzi hao waliweza kuandika baadhi ya maneno kwa herufi kubwa na kushindwa maneno mengine. Kati yao, wapo waliochanganya herufi kubwa na ndogo na wengine kutenganisha silabi moja na nyingine katika neno.

Kielelezo Na. 17 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.



2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.

(a) juisi JUISI

(b) maji MaJi

(c) asha ASHA

(d) faida fAiDA

(e) gurudumu GuruDuMu

(f) papai PAPAi

(g) zabibu ZABiBu

(h) dodoma DODOMA


(i) nanasi NANASi

(j) mwanza MWANZA

**Kielelezo Na. 17**: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani

Katika Kielelezo Na. 17, mwanafunzi aliweza kuandika maneno matatu kwa herufi kubwa kati ya maneno 10. Maneno hayo ni katika kipengele (c), (h) na (j). Aidha, katika kipengele (a), (b), (d), (e), (f), (g) na (i) alichanganya herufi kubwa na ndogo. Hivyo alipata utendaji wa wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 2,974 (10.85%) walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi hao, walikuwa na umahiri katika kuumba herufi kubwa na hivyo waliweza kuandika maneno kwa herufi kubwa na kushindwa maneno machache. Kielelezo Na. 18 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.



2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.

(a) juisi JUISI
(b) maji MAji
(c) asha ASHA
(d) faida FAiDA
(e) gurudumu GURUDUMU
(f) papai PAPAI
(g) zabibu ZABiBU
(h) dodoma DODOMA
(i) nanasi NANASI
(j) mwanza MWANZA

**Kielelezo Na. 18**: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri

Kielelezo Na. 18 kinaonesha kuwa mwanafunzi aliweza kuandika herufi kubwa katika kipengele (c), (e), (f), (h), (i), na (j). Hata hivyo, alishindwa kipengele (a), (b), (d) na (g) ambapo aliandika maneno hayo kwa kuchanganya na herufi ndogo.

Aidha, wanafunzi 3,977 (14.51%) waliweza kuandika maneno kwa herufi kubwa kwa usahihi katika vipengele vyote kumi (10). Hivyo, walikuwa na utendaji mzuri sana. Kielelezo Na. 19 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.

2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.

(a) juisi JUISI

(b) maji MAJI

(c) asha ASHA

(d) faida FAIDA

(e) gurudumu GURUDUMU

(f) papai PAPAI

(g) zabibu ZABIBU

(h) dodoma DODOMA

(i) nanasi NANASI

(j) mwanza MWANZA


**Kielelezo Na. 19**: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana

Kielelezo Na. 19 kinaonesha mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana kwa kuandika kwa usahihi maneno yote kumi (10) kwa herufi kubwa. Hii inaonesha kwamba alikuwa na umahiri wa kutosha wa kuumba maumbo ya herufi kubwa.

### 3.4.4 Swali la 3: Kunakili Kifungu cha Maneno na kuweka Alama za Uandishi

Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kunakili maneno na kuweka alama za uandishi katika nafasi zilizoachwa wazi. Alama hizo ni; nukta (.), mkato (,), kushangaa (!) na kuuliza (?). Aidha, swali lilikuwa na alama 20.

Jumla ya wanafunzi 27,412 (100%) walijibu swali hili. Kiwango cha utendaji kwa jumla kilikuwa cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 8**: *Utendaji wa wanafunzi katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa wanafunzi 5,273 (19.24%) walikuwa na utendaji mzuri sana kwa kupata alama kuanzia 16 hadi 20. Wanafunzi hao walinakili maneno yote kumi na sita (16) na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Vilevile, wanafunzi 4,409 (16.08%) waliweza kunakili baadhi ya maneno na kutumia baadhi ya alama za uandishi kwa usahihi na kupata alama kuanzia 11 hadi 15. Hivyo, walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi 1,772 (6.46%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na hivyo kuwa na utendaji wa wastani. Aidha, wanafunzi 15,958 (58.22%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5 hivyo kuwa na utendaji hafifukwa sababu walishindwa kunakili maneno kutoka kwenye kifungu cha maneno na kuandika alama za uandishi.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 15,958 (58.22%) walishindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Hivyo, walikuwa na utendaji hafifu. Hata hivyo, walikuwepo walioandika maneno yasiyoeleweka. Baadhi yao walinakili maelezo ya swali na wengine waliweka alama za uandishi bila kunakili kifungu cha maneno walichopewa. Kielelezo Na. 20 (a) na (b) vinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliopata alama za kiwango kisichoridhisha.

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Musa __ kwa nini wewe umemaliza chakula chote __ Oh __ Mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba __

.
,
!
?

**Kielelezo Na. 20 (a)**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Musa __ kwa nini wewe umemaliza chakula chote __ Oh __ Mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba __

Nukta (.)
Mkato (,)
alama ya Kushangaa (!)
alama ya kuuliza (?)

**Kielelezo Na. 20 (b):** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi

Kielelezo Na. 20 (a) na (b) kinaonesha mwanafunzi aliyetaja alama za uandishi bila kunakili kifungu cha maneno na hivyo kupata alama zisizoridhisha.

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 1,772 (6.46%) waliweza kunakili maneno 6 mpaka 10 kati ya maneno 16 waliyopewa na hivyo, kuonesha utendaji wa wastani. Kati yao, wapo walioweka alama za uandishi mahali ambapo siyo sahihi na wengine walishindwa kuunda herufi za maneno waliyopaswa kunakili.

Kielelezo Na. 21 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.


Musa __ kwa nini wewe umemaliza chakula chote __ Oh __ Mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba __

Musa_ kwaniniwewe umemaliza
chakula chote_oh_ Mimi

**Kielelezo Na. 21**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani

Katika Kielelezo Na. 21, mwanafunzi aliweza kunakili maneno 9 kati ya 16 kwa usahihi. Aidha, alishindwa kuweka alama za uandishi na hivyo kupata utendaji wa wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 4,409 (16.8%) walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi hao waliweza kupata alama 10 mpaka 15. Aidha, miongoni mwao, wapo walioweka baadhi ya alama za uandishi mahali pasipo sahihi na wengine hawakuweka kabisa. Kielelezo Na. 22 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.



3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.


Musa __ kwa nini wewe umemaliza chakula chote __ Oh __ Mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba __

MusaKwaniniweweumemalizachoKuloohn:
chote mim sikubalinitakwanda
Kusemakwamamanababa.

**Kielelezo Na. 22**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri

Kielelezo Na. 22 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyenakili maneno kumi na nne (14) na kujaza alama moja (1) ya uandishi kwa usahihi. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alishindwa kunakili maneno mawili (2) na kuweka alama tatu (3) za uandishi kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi 5,273 (19.24%) waliweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Hivyo, walikuwa na utendaji mzuri sana kwa kuwa walikuwa na umahiri katika kunakili kifungu cha maneno kumi na sita (16) na kuweka alama nne (4) za uandishi kwa usahihi. Kielelezo Na. 23 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.



3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Musa __ kwa nini wewe umemaliza chakula chote __ Oh __ Mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba __

Musa, kwa nini wewe umemaliza chakula chote? oh ! mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba .

**Kielelezo Na. 23**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana

Katika Kielelezo Na. 23, mwanafunzi aliweza kunakili kifungu chenye maneno kumi na sita (16) na kuweka alama zote nne (4) za uandishi kwa usahihi. Hivyo, kupata utendaji mzuri sana. Hii inadhihirisha kwamba wanafunzi wa kundi hili walikuwa na umahiri wa kuumba herufi kwa usahihi na kutumia alama za uandishi mahali panapostahili.


## 3.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi za Kuandika kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo (Mijini/Vijijini) na Jinsi (Wavulana/Wasichana)

Katika Stadi za Kuandika ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kimkoa, mahali shule ilipo na jinsi, ulifanyika kwa ajili ya kubainisha changamoto zilizopo na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuboresha shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.

### 3.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa kwa mwaka 2019 na 2021

Upimaji wa Stadi za Kuandika kwa mwaka 2021 ulifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara kama ilivyokuwa katika upimaji wa

mwaka 2019. Aidha, baada ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi, ulinganifu wa utendaji kimikoa ulifanyika kwa lengo la kubaini uwezo wa wanafunzi katika stadi hii. Katika kufanya ulinganifu huo, vigezo vifuatavyo vilizingatiwa: Mwanafunzi aliyepata utendaji mzuri sana (alama 38 hadi 50), mzuri (alama 26 hadi 37) wastani (alama 13 hadi 25) na hafifu (alama 0 hadi 12). Chati Na. 9 inaonesha ulinganifu wa wanafunzi kimikoa kwa mwaka 2019 na 2021.





**Chati Na. 9**: *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kimikoa kwa mwaka 2019 na 2021*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa ufaulu wa kitaifa mwaka 2021 umeshuka kwa asilimia 13.09. Mwaka 2019 ufaulu wa kitaifa ulikuwa ni asilimia 75.30 wakati mwaka 2021 ni asilimia 62.21. Aidha, mkoa ulioongoza kwa utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa miaka yote miwili ni Dar es Salaam. Hata hivyo, utendaji wa mwaka 2021 kwa mkoa huo umeshuka kwa asilimia 5.4 kutoka asilimia 95.2 mwaka 2019 hadi 89.8 mwaka 2021.

Kwa upande mwingine, mkoa wa Simiyu umekuwa na kiwango cha chini cha utendaji kwa mwaka 2021 kwa asilimia 37.94 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo mkoa huo ulikuwa na asilimia 70.40 ya ufaulu. Hivyo, mkoa huo umeshuka kwa asilimia 32.46. Aidha, mkoa wa Kigoma kwa mwaka 2019 ulikuwa na kiwango cha chini cha utendaji cha asilimia 51.9 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo mkoa huo ulikuwa na asilimia 50.6. Hivyo, mkoa huo umeshuka kwa asilimia 1.3 japokuwa umekuwa mkoa wa 19 kwa viwango vya utendaji kati ya mikoa 26 kwa mwaka 2021.

### 3.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi za Kuandika kwa Kuzingatia Mahali Shule Zilipo

Utendaji wa wanafunzi ulilinganishwa kwa kuzingatia mahali shule zilipo (mijini na vijijini). Takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi 27,412 walifanyiwa upimaji kwa mwaka 2021. Kati yao, wanafunzi 13,725 walitoka shule za mijini na 13,687 shule za vijijini. Lengo la kufanya ulinganifu lilikuwa ni kubaini viwango vya utendaji kati ya shule za mjini na vijijini ili kubaini changamoto na kuboresha viwango hivyo vya utendaji. Chati Na. 10 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi wa shule za mijini na vijijini.





**Chati Na. 10**: *Utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini*

Chati Na. 10, inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi wa shule za mijini na vijijini. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa kulikuwa na tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wa mijini na vijijini. Shule za mijini zilikuwa na utendaji mzuri wa asilimia 69.90 na shule za vijijini zilikuwa na utendaji wa asilimia 54.50.

### 3.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi

Jumla ya wanafunzi 27,412 walifanyiwa upimaji katika Stadi ya Kuandika mwaka 2021. Takwimu zinaonesha kuwa wavulana walikuwa 13,403 na wasichana 14,009. Lengo la kufanya ulinganifu wa utendaji kijinsi lilikuwa ni kubaini viwango vya utendaji kati yao ili kuinua viwango vya utendaji kwa kuzingatia usawa. Chati Na. 11 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wavulana na wasichana.




**Chati Na. 11**: *Ulinganifu wa utendaji kwa kuzingatia jinsi*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa wasichana walikuwa na utendaji mzuri wa asilimia 66.7 ikilinganishwa na wavulana waliokuwa na asilimia 57.89. Hivyo, utendaji wa wasichana ulikuwa ni mzuri zaidi ikilinganishwa na wavulana kwa tofauti ya asilimia 8.81.

## 3.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi za Kuandika

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 17,053 (62.21%) waliofanyiwa upimaji wa Stadi za Kuandika walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha, katika maswali matatu yaliyoulizwa, umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha ulikuwa mzuri zaidi ikilinganishwa na umahiri wa kuandika herufi kubwa na kunakili kifungu cha maneno pamoja na kuweka alama sahihi za uandishi.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 19,430 (70.88%) walikuwa na umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha hizo. Wanafunzi hao waliweza kuandika majina sahihi ya picha tatu (3) hadi kumi (10). Hivyo kuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Vilevile, wanafunzi 9,775 (35.66%) walikuwa na umahiri wa kuandika maneno kwa herufi kubwa. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika kuumba herufi kubwa hivyo waliweza kuandika maneno matatu (3) hadi maneno kumi (10) kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi 11,454 (41.78%) waliweza kunakili maneno sita (6) hadi kumi na sita (16) kutoka katika kifungu cha maneno na kuweka

alama za uandishi moja (1) hadi nne (4) kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana.

# SURA YA NNE

## UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo ya upimaji wa Stadi za Kuhesabu uliofanyika kwa wanafunzi wa Darasa la Pili wa mwaka 2021. Aidha, inajumuisha maelezo kuhusu muundo wa karatasi za upimaji, vigezo vya utendaji na utendaji wa jumla wa wanafunzi. Pia, inaeleza maeneo ambayo wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri sana, mzuri, wastani na hafifu. Zaidi ya hayo, katika sura hii ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia jinsi, mahali shule ilipo na mikoa umewasilishwa. Pamoja na hayo, sura hii imehitimishwa kwa muhtasari wa uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kuhesabu.

### 4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji

Umahiri wa wanafunzi katika Stadi za Kuhesabu ulipimwa katika karatasi za *STADI YA KUSOMA NA KUHESABU* na *STADI YA KUHESABU*. Karatasi ya Kwanza ilikuwa na maswali 10 yenye jumla ya alama 20. Maswali hayo yalipima umahiri wa wanafunzi katika kujumlisha na kutoa namba nzima zisizozidi 999. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kwa mdomo. Msimamizi wa upimaji alirekodi alama za mwanafunzi kwenye fomu maalum (skeli ya upimaji) ya kujaza alama za wanafunzi. Wasimamizi wengine walikuwa na vishikwambi, hivyo alama hizo zilidakwa moja kwa moja kwenye mfumo maalum wa kutunza kumbukumbu.

Karatasi ya Pili ilikuwa na maswali 10 ambayo yalipima uwezo wa wanafunzi kutambua namba zinazokosekana kwenye mfululizo na kufumbua mafumbo. Katika karatasi hiyo, wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kwa kuandika majibu kwenye nafasi wazi. Kila swali katika umahiri wa kutambua namba zinazokosekana katika mfululizo lilikuwa na alama 2, wakati kila swali kwenye umahiri wa kufumbua mafumbo lilikuwa na alama 4 na kufanya jumla ya alama 30. Hivyo, jumla ya alama katika karatasi zote mbili zilikuwa 50.

### 4.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi za Kuhesabu

Vigezo vya utendaji wa mwanafunzi vilivyotumika katika upimaji wa Stadi za Kuhesabu, kwa kila umahiri vimegawanyika katika viwango vinne kama ifuatavyo: utendaji hafifu kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali lolote au aliyeweza kujibu kwa usahihi swali moja (1) au mawili (2) tu; utendaji wa wastani kwa mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi maswali matatu (3); utendaji mzuri kwa mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi maswali manne (4); na utendaji mzuri sana kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano (5).

### 4.4 Utendaji wa Jumla katika Stadi za Kuhesabu

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 27,770 kati ya 32,216 walifanya upimaji wa Stadi za Kuhesabu. Hii inaonesha kuwa wanafunzi 4,446 (13.8%) hawakufanya upimaji. Idadi na asilimia ya wanafunzi wenye utendaji hafifu, wastani, mzuri na mzuri sana kwa kila umahiri imeoneshwa katika Jedwali Na.5.

**Jedwali Na. 5: Utendaji wa Jumla katika Stadi za Kuhesabu**

| Umahiri Uliopimwa | Utendaji wa Wanafunzi | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu | | Wastani | | Mzuri | | Mzuri Sana | |
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Kutambua Namba zinazokosekana | 16,524 | 60.72 | 4880 | 17.93 | 2234 | 8.21 | 3576 | 13.14 |
| Kujumlisha | 9,807 | 35.32 | 5,102 | 18.37 | 5,130 | 18.47 | 7,731 | 27.84 |
| Kutoa | 11,945 | 43.01 | 5,895 | 21.23 | 5,122 | 18.44 | 4,808 | 17.31 |
| Kufumbua Mafumbo | 11,776 | 43.27 | 4,946 | 18.17 | 4,549 | 16.72 | 5,943 | 21.84 |

Katika Jedwali Na. 5, asilimia 60.72, 35.32, 43.02 na 43.27 ya wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi maswali matatu hadi matano katika kutambua namba zinazokosekana, kujumlisha, kutoa na kufumbua mafumbo, mtawalia. Kwa ujumla wanafunzi walikuwa na kiwango cha utendaji mzuri sana katika umahiri wa Kujumlisha (27.84%), Kutoa (17.31%) na Kufumbua Mafumbo (21.84%). Kwa upande mwingine

wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu (60.72%) katika umahiri wa kutambua namba zinazokosekana.


## 4.5 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi kwa kila Umahiri

Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi kwa kila Umahiri umefanyika ili kuonesha asilimia ya wanafunzi ambao walijibu kila swali kwa usahihi. Katika kila umahiri utendaji wa wanafunzi ulichambuliwa kwa kuzingatia utendaji mzuri sana, mzuri, wastani na hafifu. Zaidi ya hayo, uchambuzi unajumuisha vielelezo vinavyoonesha majibu ya wanafunzi ili kuthibisha maelezo kuhusu majibu hayo.

Katika umahiri wa kujumlisha na kutoa, wanafunzi 18,088 (65.10%) walijibu maswali yote kwa kuhesabu vidole vya mikono au kutali wakati wa kutafuta majibu sahihi. Aidha, wanafunzi 18,581 (66.90%) walitumia karatasi na penseli wakati wanafunzi 4,012 (14.4%) walijibu maswali yote kwa kichwa.

### 4.5.1 Umahiri wa Wanafunzi wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mfululizo wa Namba

Umahiri wa wanafunzi wa kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba ulipimwa katika swali la 1 hadi 5 katika karatasi ya *STADI YA KUHESABU*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali hayo kwa kuandika majibu kwenye nafasi zilizoachwa wazi. Swali la 2, 4 na 5 yalihusu mfululizo wa namba unaoongezeka wakati swali la 1 na 3 yalihusu mfululizo wa namba unaopungua. Chati Na. 12 inaonesha asilimia ya wanafunzi waliojibu kila swali kwa usahihi.





**Chati Na. 12:** *Asilimia ya wanafunzi walioweza kutambua namba inayokosekana kwenye mfululizo wa namba*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa asilimia 47.8 ya wanafunzi waliofanya upimaji walijibu swali la 1 kwa usahihi. Aidha, asilimia 39.7 walipata jibu sahihi katika swali la 5. Kwa kuzingatia muundo wa maswali hayo, ni dhahiri kuwa wanafunzi hao waliweza kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba ambazo zinazotofautiana kwa 1.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2, 3 na 4 ulikuwa hafifu. Wanafunzi wengi walishindwa kubaini kuwa namba zinazofuatana kwa kila mfululizo katika maswali hayo zinatofautiana kwa 2 au 5.

Katika umahiri huu, wanafunzi 1,845 (6.78%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi hawa waliweza kubaini iwapo mfululizo wa namba unaongezeka au kupungua; na tofauti ya namba zinazofuatana kwa kila mfululizo. Pia, waliweza kufanya matendo ya kujumlisha au kutoa namba. Katika swali la 1 na 3, wanafunzi walipunguza 1 na 2 mtawalia kutoka katika namba iliyoandikwa kabla ya nafasi iliyoachwa wazi. Hivyo, walipata namba zinazokosekana kwa swali la 1 na 3 kuwa ni 3 na 6 mtawalia. Aidha, wanafunzi walitambua namba inayokosekana katika swali la 2 kuwa ni 11 baada ya kujumlisha 9 na 2. Vilevile, walitambua namba inayokosekana katika swali la 4 kuwa ni 25 baada ya kujumlisha 20 na 5.



Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi katika swali la 1 hadi la 5.

1. 6, 5, 4, 3, 2, 1
2. 3, 5, 7, 9, 11
3. 14, 12, 10, 8, 6
4. 5, 10, 15, 20, 25, 30, 35.
5. 110, 111, 112, 113.

**Kielelezo Na. 24:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana

Kielelezo Na. 24 kinaonesha kuwa mwanafunzi aliweza kutambua namba inayokosekana katika kila mfululizo. Mathalani, mwanafunzi alibaini namba inayokosekana katika swali la 5 kuwa ni 112 baada ya kujumlisha 1 na 111 au kutoa 1 kutoka 113.

Jumla ya wanafunzi 1,731 (6.36%) walikuwa na utendaji mzuri kwani waliweza kujibu maswali manne (4) kwa usahihi. Aidha, wanafunzi 2,234 (8.21%) walikuwa na utendaji wa wastani kwani waliweza kujibu maswali matatu (3) kwa usahihi. Wengi wao waliweza kutambua iwapo swali linahusu mfululizo wa kuongezeka au kupungua. Hata hivyo, baadhi yao walifanya makosa kwa kudhani kuwa mfululizo wa namba uliotolewa katika swali la 2 unapungua kwa 2 na mfululizo wa namba uliotolewa katika swali la 3 unaongezeka kwa 2 badala ya kupungua kwa 2.


Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi katika swali la 1 hadi la 5.


1. 6, 5, 4, 3, 2, 1
2. 3, 5, 7, 9, 8
3. 14, 12, 10, 8, 9
4. 5, 10, 15, 20, 25, 30, 35.
5. 110, 111, 112, 113.

**Kielelezo Na. 25:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani

Katika Kielelezo Na. 25, mwanafunzi alifanya makosa katika kujibu swali la 2 na 3 kwa kuchukulia kuwa tofauti ya namba zinazofuatana ni 1 badala ya 2 au 5.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 21,404 (78.65%) walikuwa na utendaji hafifu. Wengi wao hawakuzingatia muundo wa mfululizo wa namba katika swali husika. Hivyo, walifanya tendo la kujumlisha badala ya kutoa au kutoa badala ya kujumlisha. Wanafunzi wengine waliandika namba inayokosekana kwa kujumlisha namba ya kwanza katika mfululizo uliotolewa na tofauti ya namba hizo. Kwa mfano, katika swali la kwanza mwanafunzi mmoja aliandika 7 baada ya kujumlisha 1 kwenye 6.

Wengine walijumlisha tofauti kwenye namba ya mwisho katika mfululizo ili kupata namba inayokosekana. Kwa mfano, katika swali la 4 mwanafunzi mmoja alijumlisha 5 kwenye 35 na kupata 40 badala ya kujumlisha 5 kwenye 20 ili kupata 25. Pia, wapo wanafunzi waliojumlisha namba zote ama zilizopo kabla ya nafasi iliyoachwa wazi au namba zote zilizopo kwenye mfululizo. Kwa mfano, katika swali la 2 mwanafunzi mmoja alijumlisha 2, 5, 7 na 9 na kupata 25 badala ya kujumlisha 2 kwenye 9 ili kupata 11 ambalo ni jibu sahihi. Aidha, baadhi ya wanafunzi hawakujua matakwa ya maswali. Kwa hiyo, hawakujibu maswali au waliandika majibu ambayo hayahusiani na mfululizo wa namba uliotolewa katika swali. Mfano wa majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na ufaulu hafifu umeoneshwa kwenye Kielelezo Na. 26.


Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi katika swali la 1 hadi la 5.

1. 6, 5, 4, 5, 2, 1
2. 3, 5, 7, 9, 10
3. 14, 12, 10, 8, 9
4. 5, 10, 15, 20, 31, 30, 35.
5. 110, 111, 112, 113.

**Kielelezo Na. 26:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji hafifu

Kielelezo Na. 26 kinaonesha jinsi mwanafunzi alivyotafuta namba zinazokosekana kwa kuongeza 1 katika namba ya kabla au baada ya nafasi iliyoachwa wazi. Kwa mfano, katika swali la 4 aliongeza 1 kwenye 30 badala ya kupunguza 5 kutoka 30 au kuongeza 5 kwenye 20 ili kupata jibu sahihi ambalo ni 25.

### 4.5.2 Umahiri wa Wanafunzi katika Kujumlisha


Umahiri wa wanafunzi katika kujumlisha namba ulipimwa kwa kutumia maswali matano. Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali hayo kwa mdomo. Mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi maswali manne ya mwanzo ya kujumlisha alielekezwa kuendelea kujibu maswali ya kutoa. Maswali hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Maswali ya Kujumlisha**

| Namba ya Swali | Swali |
|---|---|
| 1. | 7 + 2 ☐ |
| 2. | 14 + 5 = ☐ |
| 3. | 21 + 32 = ☐ |
| 4. | 39 + 52 = ☐ |
| 5. | 53 + 27 = ☐ |

Katika Jedwali Na. 6 yapo maswali matano. Swali la 1, 2 na 3 yalipima uwezo wa wanafunzi katika kujumlisha namba mbili bila kubeba. Swali la 1 lilihusu namba zenye tarakimu moja, swali la 2 lilihusu namba yenye tarakimu mbili na namba yenye tarakimu moja na swali la 3 lilihusu namba zenye tarakimu mbili. Kwa upande mwingine, swali la 4 na 5 yalipima uwezo wa wanafunzi katika kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kwa kubeba.

Chati Na. 13 inaonesha utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa kujumlisha.




**Chati Na. 13**: *Asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali ya kujumlisha namba*


Chati Na.13 inaonesha kuwa asilimia 78.61 ya wanafunzi waliweza kujibu swali la 1 kwa usahihi, yaani 7 + 2 = 9. Hali kadhalika wanafunzi wengi (62.12%) waliweza kujibu swali la 2 kwa kutamka 14 + 5 = 19. Ufaulu huu mzuri unaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na uwezo mzuri katika kujumlisha namba bila kubeba. Zaidi ya hayo, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa wa wastani katika swali la 3 ambapo asilimia 43.37 ya wanafunzi waliweza kujumlisha 21 na 32 ili kupata 53.

Kwa upande mwingine, asilimia 25.40 ya wanafunzi walitamka kwa usahihi kuwa 39 + 52 = 91 katika swali la 4 wakati katika swali la 5 asilimia 22.02 ya wanafunzi walitamka kwa usahihi kuwa 53 + 27 = 80 jambo linaloonesha utendaji hafifu. Utendaji hafifuwa wanafunzi ulisababishwa na kushindwa kubeba fungu la kumi kutoka kwenye mamoja kwenda kwenye makumi. Kwa mfano, katika swali la 4 wanafunzi wengi walitamka kuwa 39 + 52 = 81 badala ya 39 + 52 = 91 na katika swali la 5 walitamka kuwa 53 + 27 = 70 badala ya 53 + 27 = 80. Aidha, baadhi ya wanafunzi hawakutoa jibu lolote, jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na umahiri wa kujumlisha.

### 4.5.3 Umahiri wa Wanafunzi katika Kutoa

Umahiri wa kutoa namba ulipimwa katika swali la 6 hadi 10 katika karatasi ya *STADI YA KUSOMA NA KUHESABU*. Wanafunzi

walitakiwa kujibu maswali hayo kwa kutamka kwa sauti. Maswali nambari 6, 7 na 8 yalihusu kutoa bila kuchukua fungu moja la kumi kutoka kwenye makumi kwenda kwenye mamoja, wakati swali la 9 na 10 yalihusisha kuchukua. Swali la 6 lilikuwa na namba mbili ambapo kila namba iliundwa kwa tarakimu moja. Swali la 7 lilikuwa na namba mbili, namba moja iliundwa kwa tarakimu mbili wakati nyingine ikiundwa kwa tarakimu moja. Swali la 8, 9 na 10 yalikuwa na namba mbili ambapo kila namba iliundwa kwa tarakimu mbili. Chati Na. 14 inaonesha asilimia ya wanafunzi waliojibu swali lililohusu kutoa namba kwa usahihi.




**Chati Na. 14**: *Asilimia ya wanafunzi waliofanya kwa usahihi tendo la kutoa namba*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa asilimia 68.59 ya wanafunzi walijibu swali la 6 kwa usahihi kwani walitamka kuwa 8 – 3 = 5. Utendaji wa wanafunzi katika kujibu swali hili ulikuwa wa juu zaidi ikilinganishwa na maswali mengine katika umahiri huu. Pia, asilimia 54.61 ya wanafunzi walijibu swali la 7 kwa usahihi kuwa 18 – 7 = 11. Aidha, asilimia 32.02 ya wanafunzi walijibu swali la 8 kwa usahihi kwa kutamka kuwa 46 – 32 = 14. Kwa kulinganisha utendaji katika maswali nambari 6, 7 na 8 ni dhahiri kuwa wanafunzi wengi walikuwa mahiri katika kutoa namba zenye tarakimu moja. Hata hivyo, baadhi yao walishindwa kutoa namba yenye tarakimu moja kutoka katika namba yenye tarakimu mbili au kutoa namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja. Kwa mfano, katika swali la 7 wanafunzi walitamka kuwa 18 – 7 = 68 badala ya 11.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 9 na la 10 ulikuwa hafifu. Asilimia 18.29 ya wanafunzi walijibu swali la 9 kwa usahihi kwa kutamka kuwa 47– 28 = 19. Aidha, asilimia 14.07 walijibu swali la 10 kwa usahihi kwa kusema kuwa 60 – 32 = 28. Hivyo, ni dhahiri kuwa wanafunzi wengi hawakuwa mahiri katika dhana ya kuchukua katika kutoa namba. Kwa mfano, katika swali la 9 baadhi ya wanafunzi walitamka kuwa 47 – 28 = 29 badala ya 19 na katika swali la 10 walijibu kuwa 60 – 32 = 38 badala ya 28.


### 4.5.4 Umahiri wa Wanafunzi katika Kufumbua Mafumbo

Uwezo wa wanafunzi katika kufumbua mafumbo ulipimwa katika swali la 6 hadi 10. Maswali hayo yameoneshwa kwenye Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na. 7: Umahiri wa Kufumbua Mafumbo**

| Namba ya Swali | Swali |
|---|---|
| 6. | Kuku alitaga mayai 7. Ikiwa mayai 2 yalivunjika, je, yalibaki mayai mangapi? |
| 7. | James alikuwa na mbuzi 6. Aliongezewa mbuzi 2 na baba yake. Je, jumla ana mbuzi wangapi? |
| 8. | Juma alichuma maembe 30. Asha alichuma maembe 40. Jumla walichuma maembe mangapi? |
| 9. | Asha alipewa pipi 44 na baba yake. Iwapo aliongezewa pipi 17 na dada yake, je, atakuwa na jumla ya pipi ngapi? |
| 10. | Kuku ana vifaranga 54. Vifaranga 26 vililiwa na mwewe. Je, alibakiwa na vifaranga vingapi? |

Maswali hayo yalipima umahiri wa wanafunzi katika kufumbua mafumbo yanayohusu maisha ya kila siku kwa kutumia dhana ya kujumlisha au kutoa namba nzima. Utendaji wa wanafunzi katika umahiri huu umeoneshwa kwenye Chati Na. 15.





**Chati Na. 15**: *Asilimia ya wanafunzi waliofumbua mafumbo yaliyotolewa kwa usahihi*

Chati Na. 15 inaonesha kuwa asilimia 59.0 ya wanafunzi walijibu swali la 7 kwa usahihi wakati asilimia 57.0 walijibu swali la 8 kwa usahihi. Pia, asilimia 54.6 ya wanafunzi walijibu kwa usahihi swali la 6. Aidha, wanafunzi wachache walifumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa katika swali la 9 na la 10. Wanafunzi waliojibu maswali haya kwa usahihi walikuwa asilimia 30.1 na 23.0 mtawalia.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, kati ya wanafunzi 27,214 waliopimwa katika umahiri wa kufumbua mafumbo, wanafunzi 11,028 sawa na asilimia 40.53 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana wakati wanafunzi 16,186 (59.48%) walikuwa na utendaji hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi waliofanya vizuri katika umahiri wa kufumbua mafumbo waliweza kutafsiri kwa usahihi maneno kama vile “aliongezewa”, “alibakiwa”, “yalibaki” na “jumla” katika matendo ya kujumlisha na kutoa. Hivyo, wanafunzi hao waliweza kufumbua mafumbo yaliyotolewa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 27.



6. Kuku alitaga mayai 7. Ikiwa mayai 2 yalivunjika, je, yalibaki mayai mangapi?

7 − 2 = 5

7. James alikuwa na mbuzi 6. Aliongezewa mbuzi 2 na baba yake. Je, jumla ana mbuzi wangapi?

6 + 2 = 8

8. Juma alichuma maembe 30. Asha alichuma maembe 40. Jumla walichuma maembe mangapi?

30 + 40 = 70

9. Asha alipewa pipi 44 na baba yake. Iwapo aliongezewa pipi 17 na dada yake, je, atakuwa na jumla ya pipi ngapi?

44 + 17 = 61


10. Kuku ana vifaranga 54. Vifaranga 26 vililiwa na mwewe. Je, alibakiwa na vifaranga vingapi?

54 − 26 = 28

**Kielelezo Na. 27:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa

Katika Kielelezo Na. 27, mwanafunzi aliweza kufumbua mafumbo yaliyotolewa kwa usahihi. Hivyo, aliandika 5, 8, 70, 61 na 28 ambayo ni majibu ya maswali nambari 6, 7, 8, 9 na 10 mtawalia. Aidha, mwanafunzi alimudu kufanya hesabu za mafumbo yaliyohitaji kubeba au kuchukua.

Wanafunzi wengine walijibu maswali yote ya mafumbo kwa kutali wakati wa kutafuta majibu sahihi. Kielelezo Na. 28 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi kutoka katika kundi hili.



6. Kuku alitaga mayai 7. Ikiwa mayai 2 yalivunjika, je, yalibaki mayai mangapi? 5

0000000=5

7. James alikuwa na mbuzi 6. Aliongezewa mbuzi 2 na baba yake. Je, jumla ana mbuzi wangapi?

000000+00=8

8. Juma alichuma maembe 30. Asha alichuma maembe 40. Jumla walichuma maembe mangapi?

…+…=70

9. Asha alipewa pipi 44 na baba yake. Iwapo aliongezewa pipi 17 na dada yake, je, atakuwa na jumla ya pipi ngapi?

…+…=61

10. Kuku ana vifaranga 54. Vifaranga 26 vililiwa na mwewe. Je, alibakiwa na vifaranga vingapi?

…=28

**Kielelezo Na. 28:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu maswali ya mafumbo kwa usahihi

Katika Kielelezo Na. 28, mwanafunzi alichora vihesabio na kuvihesabu kwa kutali wakati wa kujumlisha na kutoa namba katika kufumbua mafumbo yaliyotolewa hivyo, kupata majibu sahihi.

Kwa upande mwingine, jumla ya wanafunzi 16,186 (59.48%) walikuwa na utendaji hafifukatika umahiri huu. Baadhi yao walishindwa kufumbua mafumbo yote yaliyotolewa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa majibu waliyoandika yalikuwa na kasoro zifuatazo:

(a) Kushindwa kutafsiri maneno kama vile "yalibaki", "jumla", "aliongezewa", "vililiwa" yaliyotumika kwenye mafumbo katika matendo ya kujumlisha na kutoa. Kwa mfano, katika swali la 6, baadhi ya wanafunzi walijumlisha namba walizopewa na kupata 9 badala ya mayai 5. Katika swali la 7, walipunguza 2 katika 6 na kupata 4 badala ya mbuzi 8. Katika swali la 9, walijumlisha 54 kwa 26 na kupata 80 badala ya kutoa namba walizopewa ili kupata vifaranga 28.

(b) Kukosa ujuzi wa kujumlisha na kutoa namba. Kwa mfano, katika swali la 9 wanafunzi wengi walishindwa kujumlisha kwa kubeba fungu moja la kumi kutoka kwenye mamoja kwenda kwenye makumi. Wanafunzi hawa walipata ama 44 + 17 = 511 au 44 + 17 = 51 badala ya 44 + 17 = 61. Katika swali la 10, wanafunzi walishindwa kutoa idadi ya vifaranga 26 kutoka vifaranga 54 kwa kuchukua fungu moja kutoka kwenye makumi. Wanafunzi hawa waliandika ama 54 - 26 = 32 au 54 - 26 = 38 au 54 - 26 = 710 badala ya 54 - 26 = 28.

(c) Kunakili mafumbo yaliyotolewa badala ya kuyafumbua.

(d) Kutojibu maswali au kuandika majibu yasiyohusiana na mafumbo yaliyotolewa, jambo lililodhihirisha kuwa kuna wanafunzi hawakuwa na Stadi za Kusoma na Kuandika.

Kielelezo Na. 29 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu maswali yote katika umahiri huu.

6. Kuku alitaga mayai 7. Ikiwa mayai 2 yalivunjika, je, yalibaki mayai mangapi?

7 - 2 = 2

7. James alikuwa na mbuzi 6. Aliongezewa mbuzi 2 na baba yake. Je, jumla ana mbuzi wangapi?

6 + 2 = 8

8. Juma alichuma maembe 30. Asha alichuma maembe 40. Jumla walichuma maembe mangapi?

30
-40
10

9. Asha alipewa pipi 44 na baba yake. Iwapo aliongezewa pipi 17 na dada yake, je, atakuwa na jumla ya pipi ngapi?

44
+17
21

10. Kuku ana vifaranga 54. Vifaranga 26 vililiwa na mwewe. Je, alibakiwa na vifaranga vingapi?

54
26
32

**Kielelezo Na. 29**: Sampuli ya majibu mwanafunzi aliyeshindwa kufumbua mafumbo yote


Kielelezo Na. 29 kinaonesha jinsi mwanafunzi alivyofanya makosa ya kutoa na kujumlisha namba. Kwa mfano, katika swali la 10 alitoa mamoja 6 – 4 kupata 2 badala ya 14 – 6 kupata 8 na alitoa makumi 5 – 2 kupata 3 badala ya 4 – 2 kupata 2. Katika swali la 8 alitoa namba alizopewa badala ya kujumlisha na katika swali la 9, mwanafunzi alijumlisha namba alizopewa na kupata 21 badala ya pipi 61.

## 4.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia jinsi katika kubaini namba inayokosekana katika mfululizo, kufumbua mafumbo, kujumlisha na kutoa namba ulifanyika, ili kujua tofauti ya utendaji wao katika umahiri huo.

### 4.6.1 Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia Jinsi katika Upimaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo

Uchambuzi unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 27,214 (wavulana 13,311 na wasichana 13,903) walifanya Upimaji wa maswali ya kubaini namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba na kufumbua mafumbo. Matokeo ya uchambuzi huo yameoneshwa katika Chati Na. 16.





**Chati Na. 16**: *Utendaji wa jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa jinsi*

Chati Na. 16 inaonesha kuwa, asilimia 48.35 ya wavulana walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika umahiri wa kutambua namba katika mfululizo ikilinganishwa na asilimia

47.66 ya wasichana. Aidha, wavulana na wasichana walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 51.65 na 52.66, mtawalia, katika umahiri wa kufumbua mafumbo. Hii inaonesha kuwa, wavulana walikuwa na utendaji mzuri zaidi ya wasichana katika kutambua namba inayokosekana wakati wasichana walikuwa na utendaji mzuri zaidi ya wavulana katika kufumbua mafumbo.

### 4.6.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Jinsi katika Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa

Uchambuzi unaonesha kuwa wavulana 13,617 na wasichana 14,153 walipimwa katika umahiri wa kujumlisha na kutoa. Chati Na. 17 inaonesha asilimia ya wavulana na wasichana waliojibu kwa usahihi maswali ya kujumlisha na kutoa.




**Chati Na. 17:** *Utendaji wa jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa Jinsi*


Chati Na. 17 inaonesha kuwa katika maswali ya kujumlisha, wasichana walifanya vizuri zaidi kuliko wavulana katika swali la 1, 2 na 4 wakati wavulana walifanya vizuri zaidi kuliko wasichana katika swali la 3 na la 5. Aidha, katika maswali ya kutoa, wasichana walifanya vizuri zaidi kuliko wavulana katika swali namba 6, 7, 8 na 9 wakati wavulana walifanya vizuri zaidi katika swali la 10 pekee. Hata hivyo, tofauti kati ya wavulana na wasichana ilikuwa ndogo kwa viwango vyote vya utendaji.

## 4.7 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mahali shule ilipo (mijini na vijijini) ulilenga kubaini maeneo ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii itawezesha serikali, taasisi na wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti kuboresha utendaji wa wanafunzi katika stadi za Kuhesabu katika maeneo hayo kwa kuboresha ujifunzaji na ufundishaji. Matokeo ya wanafunzi yamelinganishwa kwa kuzingatia shule za vijijini na shule za mijini. Ulinganifu umefanywa katika umahiri wa Kutambua Namba, Kufumbua Mafumbo, Kujumlisha na Kutoa. Pia, uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi umefanyika kwa kubainisha umahiri wa wanafunzi kwa kila mkoa, Tanzania Bara.

### 4.7.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini

Ulinganifu wa Utendaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo kwa kuzingatia shule za Mijini na Vijijini ulifanyika kwa kupima wanafunzi 13,687 na 13,527 kutoka shule za mijini na vijijini mtawalia. Ulinganifu wa utendaji umefanyika ili kubaini kama kuna tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wa mijini na vijijini. Matokeo ya ulinganifu yameoneshwa katika Chati Na. 18.





**Chati Na. 18**: *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini*

Takwimu katika Chati Na. 18 zinaonesha kuwa katika kila kiwango cha utendaji kuna tofauti ya utendaji wa wanafunzi wa shule za vijijini ikilinganishwa na mijini. Aidha, wanafunzi wenye

utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa shule za mijini ni asilimia 65.26 na kwa shule za vijijini ni asilimia 54.15. Hivyo, utendaji wa wanafunzi wa shule za mijini ulikuwa mzuri zaidi kuliko shule za vijijini.

### 4.7.2 Ulinganifu wa Utendaji katika Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa Namba kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini

Ulinganifu huu ulifanyika ili kubaini tofauti za utendaji kati ya wanafunzi wa shule za mijini na vijijini. Matokeo ya ulinganifu huo yameoneshwa katika Chati Na.19.





**Chati Na. 19**: *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini katika kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa*

Chati Na.19 inaonesha kuwa asilimia 39.78 ya wanafunzi wa shule za vijijini walikuwa na utendaji hafifuwakati asilimia 28.05 ya wanafunzi wa shule za mijini walikuwa na utendaji hafifu. Hii inadhihirisha kuwa, uwezo wa wanafunzi wa kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa kwa mdomo ni mzuri zaidi katika shule za mijini ikilinganishwa na vijijini.

### 4.7.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo kati ya Mwaka 2019 na 2021

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kati ya mwaka 2019 na 2021 katika kutambua namba na kufumbua mafumbo ulifanyika kwa

kila mkoa. Ulinganifu huo umezingatia idadi ya wanafunzi walioweza kujibu kwa usahihi maswali yasiyopungua 5 kati ya 10 ambao ni utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha, wanafunzi waliojibu maswali yasiyozidi 4 kwa usahihi walikuwa na utendaji hafifu. Ulinganifu wa utendaji umefanyika katika mikoa 26 yenye jumla ya wanafunzi 27,770 waliofanya upimaji huo. Matokeo ya ulinganifu huo yameoneshwa kwenye Chati Na. 20.





**Chati Na. 20:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika kutambua namba na Kufumbua mafumbo kimikoa mwaka 2019 na 2021*

Katika Chati Na. 20, inaonekana kuwa utendaji wa wanafunzi mwaka 2021 umepanda katika baadhi ya mikoa na kushuka katika mikoa mingine ikilinganishwa na mwaka 2019. Utendaji huo umepanda katika mikoa 10 na kushuka katika mikoa 16. Aidha, katika baadhi ya mikoa utendaji ulishuka kwa kiwango kikubwa kuliko mingine. Mikoa hiyo ni Morogoro, Simiyu, Geita, Ruvuma na Dodoma. Katika mikoa hii utendaji ulishuka kwa zaidi ya asilimia 10. Mikoa iliyokuwa na kiwango kidogo cha kushuka ni Arusha, Rukwa, Songwe, Shinyanga, Mara, Tanga, Pwani, Singida na Kigoma. Kiwango cha utendaji katika mikoa hii kilishuka kwa asilimia chini ya 10.

Pia Chati Na. 20 inaonesha kuwa kati ya mikoa 26 iliyofanyiwa upimaji, mikoa 3, ambayo ni Dar es Salaam, Kilimanjaro na Njombe ilikuwa na kiwango cha juu cha utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 86.05, 76.26 na 77.08 mtawalia. Kwa ujumla, wanafunzi wengi katika mikoa mingi walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Hata hivyo, wanafunzi katika mikoa miwili ambayo ni Kigoma na Simiyu walikuwa na kiwango cha juu cha utendaji hafifukwa asilimia 33.65 na 41.46 mtawalia.

### 4.7.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa katika Kujumlisha na Kutoa Namba kati ya Mwaka 2019 na 2021

Katika eneo hili ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulizingatia upimaji kwa wanafunzi wa Darasa la Pili 2019 na 2021. Pia, ulinganifu ulihusisha idadi ya wanafunzi waliopata kuanzia alama 10 hadi 20 katika kujumlisha na kutoa. Utendaji wa wanafunzi katika mwaka 2019 na 2021 kwa mikoa yote ya Tanzania Bara umewasilishwa katika Chati Na. 21.




**Chati Na. 21:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika kujumlisha na kutoa kimikoa*

Chati Na. 21 inaonesha kuwa katika upimaji wa mwaka 2021 mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na kiwango cha juu zaidi cha utendaji ikilinganishwa na mikoa mingine. Katika mkoa huo, asilimia 91.58 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi

mzuri sana. Mikoa mingine iliyokuwa na utendaji wa kiwango kizuri ni Kilimanjaro (83.63%), Iringa (81.80%), Morogoro (80.57%), Kagera (79.46%), Pwani (79.01%), Lindi (78.64%), Mtwara (75.74%), Arusha (75.55%) na Mwanza (72.40%). Aidha, mikoa mingine iliyokuwa na kiwango kizuri cha utendaji ni Dodoma (76.04%), Njombe (74.90%), Mbeya (73.29%), Mara (69.29%), Manyara (65.58%) na Tanga (61.79%). Mikoa mingine 10 ilikuwa na kiwango cha wastani cha utendaji. Mikoa hiyo ni Ruvuma (57.16%), Rukwa (54.22%), Singida (54.10%), Katavi (53.65%), Kigoma (53.07%), Geita (52.27%), Shinyanga (50.08%), Tabora (49.48%), Songwe (46.66%) na Simiyu (43.69%).


Ulinganifu wa kiwango cha utendaji kwa upimaji wa mwaka 2019 na 2021 unaonesha kuwa katika mwaka 2021, kiwango cha utendaji kiliongezeka katika mikoa 15 na katika mikoa mingine kilishuka. Mikoa ambayo kiwango cha utendaji kilipanda pamoja na asilimia ya ongezeko lake ni Kilimanjaro (32.52%), Iringa (26.55%), Morogoro (23.33%), Dar es Salaam (17.30%), Mtwara (20.27%), Lindi (19.70%), Njombe (16.84%) na Kagera (14.31%). Mingine iliyokuwa na ongezeko katika utendaji ni Pwani (13.86%), Dodoma (11.58%), Arusha (8.38%), Tabora (7.72%), Mara (7.56%), Manyara (5.16%) na Mwanza (1.02%).

Kwa upande wa mikoa ambayo kiwango cha utendaji kilishuka, utendaji katika mkoa wa Geita ulionekana kushuka zaidi ikilinganishwa na mikoa mingine ambapo tofauti ya ufaulu kati ya mwaka 2021 na 2019 ni asilimia 28.36. Mikoa mingine ambayo kiwango cha ufaulu kilipungua pamoja na asilimia za kupungua ni Mbeya (0.99%), Kigoma (1.86%), Tanga (5.43%), Katavi (7.80%), Shinyanga (10.56%), Songwe (11.46%), Rukwa (12.51%), Singida (13.53%), Simiyu (13.96%) na Ruvuma (16.36%).

### 4.7.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Ujumla Kimikoa Mwaka 2019 na 2021

Ulinganifu wa jumla wa utendaji wa wanafunzi kati ya mwaka 2019 na 2021 ulifanyika kwa mikoa yote 26 yenye jumla ya wanafunzi 27,770 waliofanya upimaji. Ulinganifu huo ulifanywa kwa kuzingatia wanafunzi waliopata alama 13 mpaka 50 ambao ni

utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Matokeo ya upimaji yameoneshwa katika Chati Na. 22.




**Chati Na. 22**: *Ulinganifu wa jumla wa utendaji wa wanafunzi kimikoa*

Chati Na. 22 inaonesha kuwa wastani wa utendaji wa kitaifa kwa mwaka 2021 ulikuwa asilimia 60.9 ikilinganishwa na asilimia 64.20 ya mwaka 2019. Wanafunzi kutoka mikoa 5 kati ya 26, ambayo ni Dar es Salaam, Kilimanjaro, Iringa, Njombe na Kagera walikuwa na kiwango cha juu cha ufaulu wa utendaji wa wastani hadi mzuri sana ambao ni asilimia 88.4, 82.0, 77.6, 77.1 na 74.4, mtawalia. Mwaka 2019 mikoa iliyokuwa na wanafunzi wengi

wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana ilikuwa Morogoro (87.30%), Dar es Salaam (83.20%), Ruvuma (76.71%), Dodoma (75.50%) na Pwani (73.50%). Kwa matokeo haya, Dar es Salaam iliendelea kuwa miongoni mwa mikoa mitano iliyofanya vizuri katika upimaji wa mwaka 2021 na mwaka 2019. Hali kadhalika, utendaji wa wanafunzi katika mikoa ya Tanga na Manyara uliendelea kuwa juu ya wastani wa utendaji wa kitaifa wakati ule wa mikoa ya Mwanza, Mbeya na Mtwara ukipanda juu ya wastani wa utendaji kitaifa kwa mara ya kwanza. Aidha, utendaji wa wanafunzi katika mikoa ya Morogoro, Dodoma na Pwani umeshuka kwa asilimia 14.7, 4.9 na 7.1 mtawalia wakati katika mkoa wa Ruvuma umeshuka kwa kiasi kikubwa cha asilimia 17 ambao ni chini ya wastani wa utendaji wa kitaifa.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walikuwa na utendaji hafifukatika mikoa ya Simiyu (37.9%), Kigoma (38.2%), Shinyanga (41.5%), Rukwa (42.1%) na Katavi (44.8%). Mwaka 2019, mikoa iliyokuwa na wanafunzi wachache wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana ilikuwa Rukwa (41.5%), Kigoma (19.4%), Mara (52.5%), Songwe (53.9%) na Katavi (54.6%). Hivyo, mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi iliendelea kuwa na wanafunzi wachache wenye utendaji wastani hadi mzuri sana.

## 4.8 Muhtasari wa Utendaji katika Stadi za Kuhesabu

Katika upimaji wa Stadi za Kuhesabu umahiri wa wanafunzi ulipimwa kwa maswali katika dhana nne. Dhana hizo ni Kutambua Namba inayokosekana katika Mfululizo, Kufumbua Mafumbo, Kujumlisha na Kutoa.

Katika uchambuzi uliofanyika kwenye umahiri wa kutambua namba inayokosekana kwenye mfululizo, imeonekana kuwa wanafunzi walikuwa na utendaji hafifuwa asilimia 39.28. Wanafunzi hao waliweza kujibu maswali ambayo yalikuwa na mfululizo unaoongezeka au kupungua kwa 1 pekee. Aidha, walishindwa kujibu maswali ambayo mfululizo uliongezeka au kupungua kwa 2 au 5. Hii inadhihirisha kuwa, hawakuwa na umahiri wa kutafuta namba zinazokosekana katika mfululizo ambao unaongezeka au kupungua kwa kiasi kingine tofauti na 1.

Katika maswali ya kujumlisha, utendaji wa wanafunzi ulikuwa mzuri kwa asilimia 64.68. Katika eneo hili wanafunzi waliweza kujibu vizuri zaidi

maswali ambayo hayakuhusisha kubeba namba. Hata hivyo, utendaji wa wanafunzi katika kujibu maswali yaliyohusu kubeba namba ulikuwa wa kiwango cha chini, ikidhihirisha kuwa uwezo wao katika maswali hayo haukuridhisha.

Kwa upande wa maswali yaliyopima umahiri wa kutoa, asilimia 56.99 ya wanafunzi walijibu kwa usahihi, ambapo ni kiwango cha wastani cha utendaji. Wanafunzi walikuwa na ufaulu wa juu zaidi katika maswali ya kutoa namba yenye tarakimu 1 na yale ambayo hayakuhusisha kuchukua. Utendaji wa wanafunzi hao katika maswali ya kutoa namba zenye tarakimu mbili kwa kuchukua haukuridhisha.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kufumbua mafumbo, asilimia 56.73 ya wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi. Wanafunzi hao waliweza kufumbua vizuri zaidi mafumbo ambayo hayakuhusisha kubeba wala kuchukua namba. Wanafunzi walishindwa kujibu maswali hayo kwa usahihi kutokana na kukosa maarifa na ujuzi wa kufumbua mafumbo yanayohusu kubeba au kuchukua namba.

Kwa ujumla, katika Stadi za Kuhesabu wanafunzi walikuwa na kiwango kizuri cha utendaji kwani asilimia 60.90 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi walikuwa na uwezo wa kutambua namba inayokosekana katika mfululizo, kujumlisha namba zenye tarakimu moja au mbili kwa kubeba, kutoa namba zenye tarakimu moja au mbili kwa kuchukua pamoja na kufumbua mafumbo kwa usahihi. Kwa upande mwingine, asilimia 39.10 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifukutokana na kukosa umahiri wa kusoma na kuandika namba, kutokuwa na uwezo wa kujumlisha kwa kubeba na kutoa kwa kuchukua pamoja na kushindwa kufumbua mafumbo.

# SURA YA TANO

## HALI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) SHULENI

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza hali halisi ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni. Pia, inawasilisha hali ya upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na changamoto zinazojitokeza wakati wa ujifunzaji wa wanafunzi wa Stadi za KKK kwa ujumla.

### 5.2 Mbinu iliyotumika kupata Taarifa ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK

Taarifa kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) zilipatikana kwa kutumia hojaji. Hojaji hizo ziliwasilishwa kwa walimu wakuu. Lengo la hojaji hizo lilikuwa ni kubaini hali halisi ya mazingira ya kufundishia na kujifunzia, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, walimu na rasilimali nyingine. Aidha, hojaji hizo ziliandaliwa ili kubaini changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa Stadi za KKK na kupata maoni yanayolenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za hizo.

### 5.3 Taarifa Kuhusu Walimu na Wanafunzi

Uchambuzi wa hojaji unaonesha kuwa jumla ya walimu wakuu 514 (98.09%) kati ya 524 walijibu maswali yaliyoulizwa kuhusu shule zao. Walimu wakuu hao walithibitisha uwepo wa walimu 904 wanaofundisha Darasa la I na la II. Kati yao walimu 430 (47.6%) walipata mafunzo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa KKK. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, walimu waliopo katika kila shule ni kati ya mwalimu mmoja hadi walimu wanne. Walimu wakuu 375 (72.91%) walieleza kuwa idadi ya wanafunzi katika darasa ni kati ya 40 na 45. Aidha, 139 (27.09%) walieleza kuwa na idadi ya wanafunzi zaidi ya 50 kwa darasa.

### 5.4 Hali ya Upatikanaji wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Walimu wakuu walitakiwa kutoa taarifa kuhusu upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada pamoja na vifaa vya kufundishia stadi ya Kuhesabu, Kuandika na Kusoma. Hali ya upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na

kujifunzia iliainishwa katika makundi manne; hafifu, chini ya wastani, wastani, vizuri na vizuri sana kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Hali ya Upatikanaji wa Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

| Na. | Kipengele | Hafifu (%) | Chini ya wastani (%) | Wastani (%) | Vizuri (%) | Vizuri sana (%) | Idadi ya waliojibu hojaji | Jumla (%) (wastani hadi vizuri sana) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Upatikanaji wa vitabu vya kiada vya kufundishia stadi ya Kuhesabu | 4.37 | 11.43 | 47.61 | 34.51 | 2.08 | 481 | 84.20 |
| (ii) | Upatikanaji wa vitabu vya ziada vya kufundishia stadi ya Kuhesabu | 7.68 | 18.46 | 44.19 | 26.76 | 2.9 | 482 | 73.85 |
| (iii) | Uwepo wa vifaa vya kufundishia stadi ya kuhesabu (kama vile vihesabio) na vifaa vingine. | 5.04 | 10.08 | 35.5 | 43.49 | 5.88 | 476 | 84.87 |
| (iv) | Uwepo wa vifaa vya kufundishia stadi ya kuandika (kama vile vibao na vifaa vingine). | 12.06 | 19.33 | 39.5 | 25.36 | 3.74 | 481 | 68.60 |
| (v) | Uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia stadi ya Kusoma | 4.43 | 13.92 | 42.83 | 33.12 | 5.7 | 474 | 81.65 |
| (vi) | Upatikanaji wa vifaa vinavyolenga kumuendeleza mwanafunzi katika stadi ya kusoma, kama vile vitabu vya hadithi fupi. | 3.11 | 10.58 | 28.22 | 40.46 | 17.63 | 482 | 86.31 |

Jedwali Na. 8 linaonesha kuwa upatikanaji wa vifaa vya kufundishia uko katika kiwango kizuri kwa stadi zote kwa mujibu wa muhtasari wa Darasa la I na la II. Hali ya upatikanaji wa vitabu vya kiada, ziada na vifaa vingine kwa stadi zote ilikuwa nzuri kwa zaidi ya asilimia 68.60.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa upatikanaji wa vifaa vinavyolenga kumwendeleza mwanafunzi katika Stadi za Kusoma ulikuwa mzuri zaidi kwa asilimia 86.31. Kiwango hiki kimepungua kwa asilimia 9.35 ikilinganishwa na asilimia 95.66 ya upimaji wa 2019. Upatikanaji wa vifaa vya kufundishia Stadi za Kuhesabu ni mzuri kwa

asilimia 84.20. Hata hivyo, kiwango hiki kimeshuka kwa asilimia 12.87 ikilinganishwa na asilimia 89.22 ya upimaji wa 2019. Aidha, upatikanaji wa vifaa vya kuandikia ni mzuri kwa asilimia 68.60. Kiwango hiki kimepungua kwa asilimia 11.43 ikilinganishwa na asilimia 80.03 ya upimaji wa 2019. Kwa ujumla kupungua huku kumetokana na ongezeko la wanafunzi waliosajiliwa kujiunga Darasa la I mwaka 2020/2021 ambalo limetokana na mafanikio ya Sera ya Elimu Msingi bila malipo.

## 5.5 Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji KKK

Walimu wakuu waliulizwa kuhusu mazingira ya ujifunzaji wa KKK katika shule zao, majibu yao yameoneshwa katika Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9: Hali ya Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji**

| Na. | Kipengele | Hafifu (%) | Chini ya wastani (%) | Wastani (%) | Vizuri (%) | Vizuri sana (%) | Idadi ya waliojibu | Jumla (%) (Wastani hadi vizuri sana) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Uwepo wa madawati,viti na meza za kutumia walimu na wanafunzi | 1.95 | 15.96 | 39.41 | 36.48 | 6.19 | 307 | 82.08 |
| (ii) | Utoshelevu wa vyumba vya madarasa ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa darasa la I na II. | 7.42 | 19.68 | 35.81 | 31.94 | 5.16 | 310 | 72.91 |
| (iii) | Upatikanaji wa maji safi na salama ya kunywa na usafi kwa wanafunzi | 7.82 | 19.54 | 28.66 | 34.85 | 9.12 | 307 | 72.63 |

Takwimu katika Jedwali Na. 9 zinaonesha uwepo wa madawati, viti na meza za wanafunzi na walimu kuwa katika kiwango kizuri zaidi ikilinganishwa na uwepo wa vyumba vya madarasa na upatikanaji wa maji safi na salama.

Kuhusu upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama shuleni, asilimia 72.63 ya wakuu wa shule walikiri kuwepo kwa upatikanaji mzuri wa

huduma hii muhimu. Kuhusu vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa Darasa la I na la II, wakuu wa shule walibainisha kuwepo kwa utoshelevu wa asilimia 72.91. Aidha, wastani wa idadi ya wanafunzi katika Darasa ni kati ya 40 hadi 45.

## 5.6 Changamoto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK

Walimu Wakuu waliulizwa kuhusu changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK katika shule zao. Baadhi ya changamoto zilizobaishwa zimeoneshwa katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Changamoto Katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK**

| Na. | Changamoto | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Umbali kutoka nyumbani hadi shuleni. | 173 | 33.7 |
| 2. | Mahudhurio ya wanafunzi yasiyoridhisha. | 159 | 30.9 |
| 3. | Uhaba wa walimu wa Stadi za KKK. | 213 | 41.4 |
| 4. | Kupokea wanafunzi wanaohamia wenye stadi za KKK zisizoridhisha. | 148 | 28.8 |
| 5. | Uhaba wa vitendea kazi vya kufundishia na kujifunzia, kama vile vitabu n.k | 194 | 37.7 |
| 6. | Nyingine | 351 | 68.0 |

Jedwali Na. 10 linaonesha kuwa uhaba wa walimu wa Stadi za KKK ni changamoto kubwa ambayo shule zinakabiliana nayo katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi hizo.

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 41.4 ya walimu wakuu walibainisha changamoto ya uhaba wa walimu wa Stadi za KKK. Vilevile, uhaba wa vitendea kazi vya kufundishia na kujifunzia uliripotiwa na asilimia 37.7 ya walimu wakuu. Uchambuzi ulionesha pia asilimia 33.7 ya wakuu wa shule walikiri kuwa umbali wanaotembea wanafunzi kutoka nyumbani hadi shuleni na kurudi una athari kubwa katika ujifunzaji wa wanafunzi kwani huwachosha wanafunzi na wakati mwingine huwafanya wachelewe kufika shule. Aidha, asilimia 30.9 ya walimu wakuu walibainisha uwepo wa mahudhurio yasiyoridhisha ya wanafunzi na

asilimia 28.8 walibainisha kupokea wanafunzi wanaohamia wenye Stadi za KKK zisizoridhisha.

Kwa upande mwingine, walimu wakuu walitakiwa kuainisha changamoto nyingine ambazo hazikuoneshwa katika hojaji. Matokeo yanaonesha kuwa asilima 68 ya walimu wakuu walibainisha changamoto zifuatazo; athari ya lugha mama, wazazi kutotimiza majukumu yao, kuhama kwa wazazi (wanaohama kwa kudumu eneo moja kwenda jingine na wale wanaohama kulingana na msimu wa shughuli za kilimo), uhaba wa madarasa pamoja na mazingira duni wanayoishi wanafunzi husika.

Aidha, walimu wakuu walitakiwa kubainisha jambo jingine lolote ambalo halikuulizwa katika hojaji kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Katika kujibu swali hili mambo yaliyobainishwa ni pamoja na; uhaba wa walimu wa elimu maalum, kukosekana huduma mahususi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na ukosefu wa chakula shuleni. Vilevile, changamoto nyingine ni upungufu wa matundu ya vyoo na muda wa upimaji kuwa mwezi Januari badala ya mwezi Novemba au Disemba.

# SURA YA SITA

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa matokeo ya uchambuzi wa ufaulu wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Pili wa mwaka 2021. Vilevile, inatoa mapendekezo kuhusu maeneo ya kufanya maboresho na namna ya ufanyaji maboresho husika kwa wadau wa elimu wakiwemo walimu na wazazi/walezi.

### 6.2 Hitimisho

Takwimu zinaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 67.00 ya wanafunzi walifaulu.

Wanafunzi 18,911 (68.10%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika Stadi za Kusoma. Ufanisi huo ulitokana na utendaji wao wa kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha na kasi inayotakiwa. Pia, wanafunzi hao waliweza kusoma kifungu cha habari kwa ufahamu na kuweza kujibu maswali kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi 8,859 (31.90%) walikuwa na utendaji hafifu kwani walishindwa kusoma maneno yaliyoundwa na silabi zenye konsonanti mwambatano, herufi /r/ na /l/ na sauti ya king’ong’o /ng’/. Vilevile, wanafunzi wengine hawakuweza kumaliza kusoma maneno yote kwa dakika moja. Wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kusoma kifungu cha maneno kwa ufahamu na kujibu maswali.

Katika Stadi za Kuandika uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 17,053 (62.21%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kubainisha picha na kuunda maneno kwa usahihi. Hali kadhalika, waliweza kuandika maneno kwa herufi kubwa na kunakili kifungu cha maneno kwa kuweka alama sahihi za uandishi. Sambamba na hilo, wanafunzi 10,359 (37.79%) walikuwa na utendaji hafifu kwa kushindwa kubaini picha na kuandika majina ya picha walizopewa. Aidha, walishindwa kuandika maneno kwa herufi kubwa na kunakili kifungu cha maneno kwa kuandika alama sahihi za uandishi.

Takwimu zilionesha kuwa, katika Stadi za Kuhesabu wanafunzi 16,910 (60.90%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Wanafunzi

hao walikuwa na uwezo wa kujumlisha kwa kubeba na bila kubeba fungu moja la kumi kutoka kwenye makumi. Aidha, waliweza kutafsiri kwa usahihi maneno yaliyotumika kwenye mafumbo katika matendo ya kujumlisha na kutoa. Kwa upande mwingine wanafunzi 10,860 (39.1%) walishindwa kubaini namba inayokosekana katika mfululizo wa namba iliyopimwa. Wanafunzi hao walishindwa kutoa kwa kuchukua fungu moja la kumi kutoka kwenye makumi kwenda kwenye mamoja.

Takwimu za ulinganifu wa ufaulu wa Stadi za KKK kati ya shule za mijini na vijijini zilionesha kuwa shule za mijini zilikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 73.41 ikilinganishwa na shule za vijijini ambazo zilikuwa na ufaulu wa asilimia 60.60. Uchambuzi unaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa kuzingatia mikoa, mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na utendaji mzuri zaidi kwa asilimia 90.46. Aidha, mkoa huo uliongoza katika Stadi zote ambapo katika Stadi ya Kusoma ulikuwa na utendaji mzuri wa asilimia 89.2, Kuandika (89.8%) na Kuhesabu (88.4%). Mkoa wa mwisho katika Stadi ya Kusoma ulikuwa Katavi (46.07%). Aidha, mkoa wa Simiyu ulikuwa wa mwisho katika Stadi ya Kuandika na Kuhesabu kwa asilimia 37.9 mtawalia.

## 6.3 Mapendekezo

Taarifa za uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi katika Stadi zote tatu zinaonesha kushuka kwa utendaji ikilinganishwa na mwaka 2019. Ili kuimarisha utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wanaofundisha Stadi za Kusoma watafute mbinu za kuwaongoza wanafunzi kusoma maneno 50 au zaidi kwa ufasaha na kasi inayotakiwa kwa dakika moja. Wanafunzi waongozwe kusoma neno zima badala ya kusoma silabi mojamoja wakati wa kusoma kifungu cha habari ili kuelewa na kutafsiri walichokisoma. Vilevile, walimu wawaongoze wanafunzi kusoma vifungu vya habari na hadithi mbalimbali ili kujenga umahiri wa kujibu maswali ya ufahamu kwa ngazi zote. Aidha, vifungu vya habari na hadithi ziwe na maneno yenye sauti ya king’ong’o (ng’), sauti ‘r’ na ‘l’, na maneno yaliyoundwa na konsonanti mwambatano ili wanafunzi wafanye mazoezi zaidi juu ya utamkaji wa "n" na "l". Hali kadhalika, walimu wapime uwezo wa wanafunzi wa kusoma kwa

ufasaha kwa kutumia zana mbalimbali za upimaji kama vile mazoezi, majaribio na mitihani.

(b) Katika Stadi za Kuandika walimu watoe mazoezi ya kutosha yatakayowawezesha wanafunzi katika utambuzi wa picha, michoro na vitu mbalimbali vilivyopo katika mazingira yanayowazunguka na kuunda maneno. Vilevile, walimu wawawezeshe wanafunzi kuunda maneno kwa herufi kubwa na kutumia alama za uandishi mahali panapostahili wakati wa utoaji wa mazoezi na upimaji.

(c) Ili kuboresha Stadi za Kuhesabu, walimu watoe mazoezi ya kutosha katika kukamilisha mfuatano wa namba zinazoongezeka au zinazopungua kwa mbili na kuendelea, kujumlisha kwa kubeba na kutoa kwa kuchukua na kufumbua mafumbo.

(d) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa shule na Uongozi wa Elimu katika ngazi zote wafuatilie ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi hizo na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kwa lengo la kuimarisha umahiri wa wanafunzi katika stadi hizo.

(e) Vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia kama michoro ya ukutani na kadi zenye maneno zitumike ipasavyo ili kukuza msamiati na kuunda maneno. Aidha, walimu wabuni zana za kufundishia na kujifunzia zinazoakisi mazingira.

(f) Mamlaka husika ielekeze walimu, wazazi/walezi na jamii kwa ujumla kuimarisha na kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

**Kiambatisho Na. 1: Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma na Kuhesabu**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA PILI**

**STADI YA KUSOMA NA KUHESABU**

**KARATASI YA MWANAFUNZI**

**Muda: Dakika 20** **Januari 2022 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali **yote kwa mdomo**.
2. Kila mwanafunzi atapimwa kwa **dakika 20**.
3. Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi juu ya fomu maalum ya upimaji kwa **kalamu ya wino wa bluu**.
4. Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma na kujibu maswali ya ufahamu na kuhesabu, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika skeli ya upimaji kwa kutumia **kalamu ya wino mwekundu**.

Ukurasa wa 1 kati ya 4

Tina na Subira ni marafiki. Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

Ukurasa wa 2 kati ya 4

1. 7 + 2 =

2. 14 + 5 =

3. 21 + 32 =

4. 39 + 52 =

5. 53 + 27 =

6. 8 - 3 =

7. 18 - 7 =

8. 46 - 32 =

9. 47 - 28 =

10. 60 - 32 =

## Kiambatisho Na. 2: Skeli ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma na Kuhesabu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

***Fomu Maalum ya Kujaza Alama za Mwanafunzi katika Upimaji wa Kusoma na Kuhesabu***

*Jina la Mwanafunzi*______________________________

*Namba ya Mwanafunzi*____________________________

<table>
<tr><th colspan="6">KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU</th></tr>
<tr><th colspan="3">STADI YA KUSOMA</th><th colspan="3">STADI YA KUHESABU</th></tr>
<tr><th>Namba ya Swali</th><th>Alama</th><th>Saini ya Mpimaji</th><th>Namba ya Swali</th><th>Alama</th><th>Saini ya Mpimaji</th></tr>
<tr><td rowspan="5">1.</td><td rowspan="5"></td><td rowspan="5"></td><td>1.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>2.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>3.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>4.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>5.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td rowspan="5">2.</td><td rowspan="5"></td><td rowspan="5"></td><td>6.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>7.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>8.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>9.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>10.</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>Jumla ya Alama</td><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
</table>

*Ukurasa wa 1 kati ya 9*

## SEHEMU A

## 201 STADI YA KUSOMA

1. Kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha, umakini na kasi inayotakiwa (alama 25).

***Maelekezo kwa Msimamizi***

*Weka alama ya* ***mkwaju (/)*** *kwa kila neno ambalo mwanafunzi* ***ameshindwa*** *kulisoma kwenye kifungu cha maneno. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kusoma kwa usahihi, zungushia* ***(Ø)*** *neno hilo. (Kila neno* ***moja*** *sahihi* ***alama 00½****)*

(a) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika ***Skeli ya Upimaji.***

(b) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma neno baada ya **sekunde 3** mwelekeze kusoma neno linalofuata.

(c) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma **maneno yote** ya sentensi ya kwanza, sitisha zoezi na weka alama ya mabano [ ] katika neno la mwisho kusomwa kisha endelea na stadi ya kuhesabu.

(d) Iwapo mwanafunzi atasema **sijui** wakati akisoma, chukulia kama ni **kosa** kisha weka alama ya mkwaju.

(e) Iwapo mwanafunzi atashindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya **sekunde 60**, weka alama ya mabano [ ] katika neno la mwisho alilosoma.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

Karibu .........·Hujambo?

(a) Hapa kuna kifungu cha maneno, nikisema anza utasoma (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari).

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri uwezavyo.

(c) Weka kidole kwenye neno la kwanza. Je uko tayari? Anza.

Tina na Subira ni marafiki.

Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Alama:** ☐ **Muda uliotumika:** ☐

2· Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

(a) Mwongoze mwanafunzi kusoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari. Baada ya mwanafunzi kusoma ndani ya **dakika 3**, chukua karatasi ya mwanafunzi kisha muulize maswali yaliyopo kwenye **Skeli ya Upimaji**.

(b) Mwanafunzi akitoa jibu sahihi zungushia alama **5**, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0**. Endapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi na kisha kufanya marekebisho kwa kutoa jibu sahihi, weka mkwaju kwenye alama O kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali.

(c) Iwapo utamuuliza swali mwanafunzi na akashindwa kujibu ndani ya **sekunde 10**, zungushia alama O kisha endelea na swali linalofuata.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Utasoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari).

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri uwezavyo· Baada ya kusoma nitachukua karatasi yako kisha

nitakuuliza maswali yanayotokana na kifungu cha maneno ulichosoma· Je uko tayari? Anza.

Tina na Subira ni marafiki.

Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Maswali na Majibu**

| **Kipengele** | **Maswali na majibu** | **Alama** | |
|---|---|---|---|
| 1· | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2· | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3· | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4· | Subira alitumia nini kujaza maji | 5 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kwenye ndoo yake? **(Kata)** | | |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |
| **Jumla ya Alama** | | | |

## SEHEMU B

## 203 STADI YA KUHESABU

**Maelekezo kwa Msimamizi**

Zungushia alama **2** iwapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **0** iwapo atatoa jibu lisilosahihi. Iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilosahihi na kisha kufanya marekebisho na kutoa jibu sahihi, weka mkwaju kwenye alama **0** kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali.

(a) Mwongoze mwanafunzi kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa. Mpe karatasi na penseli kisha mwambie kuwa anaweza kutumia kama anataka lakini sio lazima.

(b) Iwapo mwanafunzi atatumia njia isiyoridhisha muulize kama anaweza kutumia njia nyingine.

(c) Iwapo mwanafunzi ataendelea kutumia njia isiyoridhisha au atasimama/atakwama/hatajibu kwa **sekunde 5** endelea na swali linalofuata.

(d) Sitisha zoezi endapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kujumlisha endelea na maswali ya kutoa.

(e) Iwapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kutoa sitisha zoezi· Endelea na mwanafunzi anayefuata.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Hapo kuna maswali ya kujumlisha na kutoa (mwoneshe mwanafunzi kwa mkono swali la 1 hadi la 5 kisha swali la 6 hadi 10).

(b) Utaanza na swali la 1. Utajibu maswali haya kwa mdomo. Unaweza kutumia penseli na karatasi kama unataka lakini sio lazima. Je upo tayari? Anza.

| **Na·** | **Maswali na majibu** | **Alama** | |
|---|---|---|---|
| 1· | 7 + 2 = (**9**) | 2 | 0 |
| 2· | 14 + 5 = (**19**) | 2 | 0 |
| 3· | 21 + 32 = (**53**) | 2 | 0 |
| 4· | 39 + 52 = (**91**) | 2 | 0 |
| 5· | 53 + 27 = (**80**) | 2 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | 8 - 3 = (**5**) | 2 | 0 |
| 7. | 18 - 7 = (**11**) | 2 | 0 |
| 8. | 46 - 32 = (**14**) | 2 | 0 |
| 9. | 47 - 28 = (**19**) | 2 | 0 |
| 10. | 60 - 32 = (**28**) | 2 | 0 |
| **Jumla ya Alama** | | | |

**Maoni ya msimamizi**

Weka alama ya vema (√) iwapo mwanafunzi:

- [ ] ametumia vidole au kutali.
- [ ] ametumia karatasi na penseli.
- [ ] amejibu maswali yote kwa kichwa.

## Kiambatisho Na. 3: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika

Jina la Mwanafunzi______________________

Namba ya Mwanafunzi____________________

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA ELIMU YA MSINGI DARASA LA PILI

202 STADI YA KUANDIKA

Muda: Dakika 40 Januari 2022 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina **maswali matatu**.
2. Andika **Jina lako** na **Namba yako** katika kila ukurasa.
3. Jibu maswali **yote** matatu.
4. Andika **majibu yako yote** kwa kutumia penseli.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| Jumla | | |

Ukurasa wa 1 kati ya 4

Jina la Mwanafunzi____________________

Namba ya Mwanafunzi__________________

1. **Andika** majina ya **picha** hizi :

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | <br>________________ | (b) | <br>________________ |
| (c) | <br>________________ | (d) | <br>________________ |
| (e) | <br>________________ | (f) | <br>________________ |

Ukurasa wa 2 kati ya 4

Jina la Mwanafunzi________________________

Namba ya Mwanafunzi____________________

| | | | |
|---|---|---|---|
| (g) | <br>__________________ | (h) | <br>__________________ |
| (i) | <br>__________________ | (j) | <br>__________________ |

2. **Andika** maneno yafuatayo kwa **herufi kubwa** katika nafasi iliyo wazi katika kila neno.

(a) juisi ________________________

(b) maji ________________________

Jina la Mwanafunzi____________________________

Namba ya Mwanafunzi________________________

(c) asha ______________________________

(d) faida ______________________________

(e) gurudumu ______________________________

(f) papai ______________________________

(g) zabibu ______________________________

(h) dodoma ______________________________

(i) nanasi ______________________________

(j) mwanza ______________________________

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Musa __ kwa nini wewe umemaliza chakula chote __ Oh __ Mimi sikubali nitakwenda kusema kwa mama na baba __

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

**Kiambatisho Na. 4: Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu**

Jina la Mwanafunzi________________________________
Namba ya Mwanafunzi ______________________________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA PILI**

**203** **STADI YA KUHESABU**

**Muda: Dakika 50** **Januari 2022 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (10)**.

2. Jibu maswali **yote**.

3. Andika majibu yote kwa **penseli**.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | | 6. | | |
| 2. | | | 7. | | |
| 3. | | | 8. | | |
| 4. | | | 9. | | |
| 5. | | | 10. | | |
| Jumla ya Alama | | | | | |

Ukurasa wa 1 ya kati 3

Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi katika swali la 1 hadi la 5.

1. 6, 5, 4, ____, 2, 1
2. 2, 5, 7, 9, ____
3. 14, 12, 10, 8, ____
4. 5, 10, 15, 20, ________, 30, 35.
5. 110, 111, _______, 113.

6. Kuku alitaga mayai 7. Ikiwa mayai 2 yalivunjika, je, yalibaki mayai mangapi?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

____________

7. James alikuwa na mbuzi 6. Aliongezewa mbuzi 2 na baba yake. Je, jumla ana mbuzi wangapi?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

8. Juma alichuma maembe 30. Asha alichuma maembe 40. Jumla walichuma maembe mangapi?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

9. Asha alipewa pipi 44 na baba yake. Iwapo aliongezewa pipi 17 na dada yake, je, atakuwa na jumla ya pipi ngapi?

10. Kuku ana vifaranga 54. Vifaranga 26 vililiwa na mwewe. Je, alibakiwa na vifaranga vingapi?

## Kiambatisho Na. 5: Dodoso la Mkuu wa Shule

**BARAZA LA MTIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU 2021**

**HOJAJI LA MWALIMU MKUU**

**Jina la Shule:** ..........................................................................................

**Namba ya shule:** ......................................................................................

**Mkoa:** ..............................................

**Wilaya:** ..............................................

**A: Taarifa za shule kwa ujumla**

*Tafadhali jaza taarifa kuhusu wanafunzi na walimu wa KKK katika shule yako kwa kuandika katika visanduku/sehemu zilizoachwa wazi.*

1. Kuna walimu wangapi wa darasa la 2 wanaofundisha shule hii? ☐

2. Je, kuna walimu wangapi wa darasa la pili waliopo shuleni kwa sasa? ☐

3. Je, walimu wanaofundisha stadi za kusoma Kuandika na Kuhesabu waliwahi kuhudhuria mafunzo ya stadi hizo?
   Ndiyo ☐ Hapana ☐

   Ikiwa jibu ni Ndiyo andika idadi ya waliopewa mafunzo. ☐

4. Je, kuna mikondo mingapi ya wanafunzi wa darasa la 2? ☐

5. Kuna wanafunzi wangapi wa darasa la pili walioandikishwa katika shule hii?
   Kati yao wavulana ni wangapi? ☐ na Wasichana ni wangapi? ☐

6. Je, Kuna wanafunzi wangapi waliohudhuria Shuleni leo? ☐

   Kati yao Wavulana ni Wangapi? ☐ na Wasichana ni wangapi? ☐

Je, kuna wanafunzi walioshindwa kufanya upimaji? Kama wapo waorodheshe.

| Na. | Namba ya Mwanafunzi | Sababu Ya Kutofanya Upimaji |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

**B: Taarifa kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

*Tafadhali jaza maoni yako kuhusu uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuweka alama ya vema (✓) kwenye uchaguzi unaolingana na maoni yako.*

| Na. | swali | Hafifu | Chini ya Wastani | Wastani Mzuri | Mzuri | Mzuri Sana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Upatikanaji wa vitabu vya kiada kufundishia stadi za kuhesabu shuleni kwako ni wa namna gani? | | | | | |
| (ii) | Upatikanaji wa vitabu vya ziada kwa ajili ya mazoezi ya stadi ya kuhesabu unaweza kuelezwa kuwa ni: | | | | | |
| (iii) | Uwepo wa vifaa vya kufundisha stadi ya kuhesabu (kama vile vihesabio na vifaa vingine unaweza | | | | | |

| Na. | swali | Hafifu | Chini ya Wastani | Wastani Mzuri | Mzuri | Mzuri Sana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | kuelezwa kuwa ni: | | | | | |
| (iv) | Uwepo wa vifaa vya kufundishia stadi ya kuandika (kama vile vibao na vifaa vingine) unaweza kuelezwa kuwa ni: | | | | | |
| (v) | Je, uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia stadi ya kusoma unaweza kuuelezeaje? | | | | | |
| (vi) | Je, unaweza kuelezeaje upatikanaji wa vifaa vinavyolenga kuendeleza stadi ya kusoma kama vile vitabu vya hadithi fupifupi kwa watoto wadogo? | | | | | |

**C: Taarifa kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji**

*Tafadhali jibu maswali kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwek alama ya vema (✓) kwenye kisanduku kulingana na uchaguzi wako kuhus ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK katika shule yako.*

| Na. | Swali | Hafifu | Chini ya Wastani | Wastani | Mzuri | Mzuri Sana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Uwepo wa madawati, viti na meza za kukalia wanafunzi na walimu shuleni kwako wakati wa kujifunza unaweza kuelezwa kuwa ni; | | | | | |
| (ii) | Ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | darasa la 2 waliopo shuleni kwa sasa, hali ya uwepo wa vyumba vya madarasa inaweza kuelezewa kuwa ni: | | | | | |
| (iii) | Je, upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa ajili ya kunywa wanafunzi pamoja na usafi binafsi kama vile kunawa wanapotoka shuleni unaweza kuelezewa kuwa ni: | | | | | |

**D: Changamoto zinazojitokeza wakati wa ujifunzaji wa wanafunzi wa stadi za KKK**

*Tafadhali jibu maswali kuhusu changamoto zinazojitokeza ambazo zinafanya ujifunzaji wa wanafunzi wa stadi za KKK kuwa mgumu kwa kuweka alama ya vema (✓) katika changamoto inayojitokeza zaidi. (unaweza kuweka vema kwenye changamoto zaidi ya moja).*

(i) Umbali wa wanafunzi wengi kutoka shule ilipo ☐

(ii) Wanafunzi kukosa masomo mara kwa mara kutokana na mahudhurio yasiyoridhisha ☐

(iii) Uhaba wa walimu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi ☐

(iv) Kupokea wanafunzi wanaohamia ambao stadi zao za KKK haziridhishi ☐

(v) Uhaba wa vitendea kazi kama vile vitabu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi ☐

(vi) Changamoto nyinginezo (Zitaje kama zipo) ____________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

**E: Upatikanaji na maoni kuhusu kitabu cha uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa mwaka 2019**

(i) Je, umepata kitabu chenye taarifa ya uchambuzi wa upimaji wa KKK wa mwaka 2019?

Ndiyo ☐ Hapana ☐

(ii) Je, unafikiri vitabu hivyo vya uchambuzi vimeweza kusaidia walimu katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK?

Ndiyo ☐ Hapana ☐

**F: Tarifa Nyinginezo**

Je, ni jambo gani ambalo halikuulizwa kwenye dodoso hili kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ambalo ungependa Baraza la Mitihani lifahamu? (Toa maelezo mafupi) ________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Jina Kamili la Mwalimu Mkuu ..............................................

Sahihi ....................................................

***Asante kwa Ushirikiano Wako!***